| AFRICAN UNION | | UNION AFRICAINE |
|---|---|---|
| الاتحاد الأفريقي | | UNIÃO AFRICANA |
| UMOJA WA AFRIKA | | UNIÓN AFRICANA |

**Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844**
**Website:** www.au.int


**BARAZA LA UTENDAJI**
**Mkutano wa Arobaini na nne wa Kawaida**
**15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**

**EX.CL/1492(XLIV)**
Asili: Kiingereza

# RIPOTI YA SHUGHULI YA MAHAKAMA YA AFRIKA JUU YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU (AFCHPR)

<table>
<tr><td>UMOJA WA AFRIKA</td><td rowspan="2"></td><td>UNION AFRICAINE</td></tr>
<tr><td>الاتحاد الأفريقي</td><td>UNIÃO AFRICANA</td></tr>
<tr><td colspan="3">MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU<br><br>COUR AFRICAINE DES DROITS DE L’HOMME ET DES PEUPLES</td></tr>
</table>

# RIPOTI YA SHUGHULI ZA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

## JANUARI 1 – DESEMBA 31, 2023

## I. UTANGULIZI

1. Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (hapa inajulikana kama Itifaki), iliyopitishwa mnamo Juni 1998, huko Ouagadougou, Burkina Faso, na Shirika la Umoja wa Afrika (OAU). Itifaki ilianza kutumika tarehe 25 Januari 2004.

2. Mahakama ilianza kufanya kazi mwaka 2006 na inaundwa na Majaji kumi na mmoja (11) waliochaguliwa na Baraza la Utendaji la Umoja wa Afrika. Makao makuu ya Mahakama yapo Arusha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Kifungu cha 31 cha Itifaki kinaitaka Mahakama *"…iwasilishe ripoti ya kazi yake katika kila kikao cha kawaida cha Mkutano. Ripoti hiyo kwa umahususi, itabainisha kesi ambazo Serikali haijatii hukumu ya Mahakama ".*

4. Ripoti ya sasa imewasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha Itifaki kilichotajwa hapo juu. Ripoti hii inaelezea shughuli zilizofanywa na Mahakama kuanzia tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba 2023, hasa shughuli za mahakama, utawala na utandaaji, pamoja na hatua zilizochukuliwa kutekeleza maamuzi ya Baraza la Utendaji yanayohusiana na utendaji wa Mahakama.

## II. HALI YA KURIDHIA ITIFAKI NA AMANA YA KIFUNGU CHA 34(6) AZIMIO, KUKUBALI MAMLAKA YA MAHAKAMA YA KUPOKEA KESI KUTOKA KWA WATU BINAFSI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGO)

5. Kufikia tarehe 31 Desemba 2023, Itifaki hiyo ilikuwa imeridhiwa na Nchi thelathini na nne (34) Wanachama wa Umoja wa Afrika, ambazo ni: Algeria, Benin, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Chad, Congo, Côte d'Ivoire, Komoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea-Bissau, Kenya, Libya, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mali, Mauritania, Mauritius, Msumbiji, Niger, Nigeria, Uganda, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi, Senegal, Afrika Kusini, Tanzania, Togo, Tunisia na Zambia. ***Angalia Jedwali la 1****.*

6. Kati ya Nchi Washirika wa Itifaki thelathini na nne (34), ni nane (8) tu (8) i nane tu ndizo zimeweka Azimio linalohitajika chini ya Kifungu cha 34(6), wakikubali mamlaka ya Mahakama kupokea kesi moja kwa moja kutoka kwa watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Nchi hizi ni Burkina Faso, Gambia, Ghana, Guinea-Bissau, Malawi, Mali, Niger na Tunisia. ***Angalia Jedwali la 2****.*

7. Kati ya mwaka 2016 na 2020, Nchi Nne (4) Wanachama wa Itifaki ziliondoa Azimio lao chini ya Kifungu cha 34(6). Nchi hizi ni Rwanda (2016), Tanzania (2019), Benin (2020) na Côte d'Ivoire (2020).

| **Jedwali la 1: Orodha ya Nchi Wanachama wa Itifaki** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Nchi** | **Tarehe ya Saini** | **Tarehe ya Uidhinishaji/Kukubali** | **Tarehe ya kuweka azimio** |
| **1.** | Algeria | 13/07/1999 | 22/04/2003 | 03/06/2003 |
| **2.** | Benin | 09/06/1998 | 22/08/2014 | 22/08/2014 |
| **3.** | Burkina Faso | 09/06/1998 | 31/12/1998 | 23/02/1999 |
| **4.** | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 09/09/1999 | 08/12/2020 | 08/12/2020 |
| **5.** | Burundi | 09/06/1998 | 02/04/2003 | 12/05/2003 |
| **6.** | Kameruni | 25/07/2006 | 17/08/2015 | 17/08/2015 |
| **7.** | Chad | 06/12/2004 | 27/01/2016 | 08/02/2016 |
| **8.** | Kongo | 09/06/1998 | 10/08/2010 | 06/10/2010 |
| **9.** | Cote d 'Ivoire | 09/06/1998 | 07/01/2003 | 21/03/2003 |
| **10.** | Komoro | 09/06/1998 | 23/12/2003 | 26/12/2003 |
| **11.** | Gabon | 09/06/1998 | 14/08/2000 | 29/06/2004 |
| **12.** | Gambia | 09/06/1998 | 30/06/1999 | 15/10/1999 |
| **13.** | Ghana | 09/06/1998 | 25/08/2004 | 16/08/2005 |
| **14.** | Guinea Bissau | 09/06/1998 | 3/11/2021 | 3/11/2021 |
| **15.** | Kenya | 07/07/2003 | 04/02/2004 | 18/02/2005 |
| **16.** | Libya | 09/06/1998 | 19/11/2003 | 08/12/2003 |
| **17.** | Lesotho | 29/10/1999 | 28/10/2003 | 23/12/2003 |
| **18.** | Madagaska | 09/06/1998 | 12/10/2021 | 12/10/2021 |
| **19.** | Malawi | 09/06/1998 | 09/09/2008 | 09/10/2008 |
| **20.** | Mali | 09/06/1998 | 10/05/2000 | 20/06/2000 |
| **21.** | Mauritania | 22/03/1999 | 19/05/2005 | 14/12/2005 |
| **22.** | Mauritius | 09/06/1998 | 03/03/2003 | 24/03/2003 |
| **23.** | Msumbiji | 23/05/2003 | 17/07/2004 | 20/07/2004 |
| **24.** | Niger | 09/06/1998 | 17/05/2004 | 26/06/2004 |
| **25.** | Nigeria | 09/06/2004 | 20/05/2004 | 09/06/2004 |
| **26.** | Rwanda | 09/06/1998 | 05/05/2003 | 06/05/2003 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **27.** | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi | 25/07/2010 | 27/11/2013 | 27/01/2014 |
| **28.** | Senegal | 09/06/1998 | 29/09/1998 | 30/10/1998 |
| **29.** | Afrika Kusini | 09/06/1999 | 03/07/2002 | 03/07/2002 |
| **30.** | Tanzania | 09/06/1998 | 07/02/2006 | 10/02/2006 |
| **31.** | Togo | 09/06/1998 | 23/06/2003 | 06/07/2003 |
| **32.** | Tunisia | 09/06/1998 | 21/08/2007 | 05/10/2007 |
| **33.** | Uganda | 01/02/2001 | 16/02/2001 | 06/06/2001 |
| **34.** | Zambia | 09/06/1998 | 28/12/2022 | 10/01/2023 |
| **Idaidi ya Nchi – 55** | | **Idadi ya Saini – 52** | **Idadi ya Idhini – 34** | **Idadi ya Maazimio – 34** |

Chanzo: Tovuti ya Umoja wa Afrika.

**Jedwali la 2: Orodha ya Nchi Wanachama ambazo zimeweka Azimio la Kifungu cha 34(6)**

| **Na.** | **Nchi** | **Tarehe ya Saini** | **Tarehe ya kuweka azimio** |
|---|---|---|---|
| 1. | Burkina Faso | 14/07/1998 | 28/07/1998 |
| 2. | Ghana | 09/02/2011 | 10/03/2011 |
| 3. | Malawi | 09/09/2008 | 09/10/2008 |
| 4. | Mali | 05/02/2010 | 19/02/2010 |
| 5. | Tunisia | 13/04/2017 | 29/05/2017 |
| 6. | Gambia | 23/10/ 2018 | 03/02/2020 |
| 7. | Niger | 28/10/2021 | 28/10/2021 |
| 8. | Guinea Bissau | 03/11/2021 | 03/11/2021 |
| Chanzo: Tovuti ya Umoja wa Afrika | | **Jumla** | **# Nane (8)** |

## III. MUUNDO WA MAHAKAMA

8. Katika Kikao chake cha 69 cha Kawaida kilichofanyika kuanzia tarehe 12 Juni hadi 7 Julai 2023 jijini Arusha, Tanzania, Mahakama ilifanya uchaguzi wa Mofisa wapya kama ifuatavyo: Rais – Mhe. Jaji Imani Daud Aboud, na Makamu wa Rais, Mhe. Jaji Modibo Sacko.

9. Muundo wa sasa wa Mahakama umeambatanishwa kwenye Ripoti ya sasa kama **Kiambatisho cha I.**

## IV. SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA MAHAKAMA

10. Katika kipindi kinachoripotiwa, Mahakama ilifanya shughuli kadhaa za kimahakama na pia zisizo za kimahakama.

### i. Shughuli za Kimahakama

11. Shughuli za kimahakama zinazofanywa na Mahakama, pamoja na mambo mengine zinahusiana na ufunguzi wa mwaka wa mahakama, kufanya vikao, kupokea na kushughulikia kesi zilizowasilishwa mbele yake, kupitia, *pamoja na mambo mengine*, usimamizi wa kesi, utoaji wa hukumu, maamuzi na maagizo.

12. Kuanzia tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba 2023, Mahakama ilipokea kesi mpya nane (08).

13. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006, Mahakama imepokea jumla ya Maombi mia tatu na arobaini (340) katika masuala yenye utata na Maombi kumi na tano (15) ya Maoni ya Ushauri. Mahakama imetupilia mbali jumla ya Maombi mia mbili na tano (205) na Maombi kumi na tano (15) ya Maoni ya Ushauri, na ina Maombi mia moja na thelathini na tano (135) yanayosubiri kushughulikiwa.

### a. Ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama wa 2023

14. Ili kuadhimisha Maadhimisho ya Miaka 15 mwaka 2021, Mahakama iliweka lengo lake la kuongeza kufahamika kwake na ushirika wake na wadau. Kulingana na haya, iliamua kwamb itafanya sherehe mwanzoni mwa vikao vyake vya kwanza kati ya vinne vya kawaida kila mwaka kuashiria ufunguzi rasmi wa mwaka wa mahakama. Kwa hivyo, ufunguzi wa uzinduzi wa mwaka wa kimahakama wa Mahakama ulifanyika tarehe 28 Februari 2022 katika makao makuu ya Mahakama jijini Arusha, chini ya kaulimbiu, "*Mahakama ya Afrika na Afrika Tuitakayo*", iliyoambatana na Agenda 2063, ambayo kauli mbiu yake ni "*Afrika Tuitakayo*."

15. Ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama wa 2023 ulifanyika tarehe 20 Februari 2023 chini ya mada *"Kuunganisha maamuzi ya kisheria ya mahakama za haki za binadamu za kikanda na kimataifa katika mahakama za kitaifa".* Hafla hiyo ilifanyika katika Makao Makuu ya Mahakama jijini Arusha, Tanzania. Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa hotuba kuu, baada ya Mheshimiwa Jaji Imani D. Aboud, Rais wa Mahakama ya Afrika kufungua rasmi Mwaka wa Mahakama wa 2023.

16. Hafla hiyo ilikuwa jukwaa la Mahakama kushirikiana na wadau muhimu, hasa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, vyombo vingine vya haki za binadamu vya Umoja wa Afrika, mahakama zingine za haki za binadamu za kikanda, watendaji wa serikali na wasio wa serikali, kutafakari, kubadilishana mawazo na kuangazia kazi ya Mahakama ya Afrika kwa mwaka husika.

17. Kama sehemu ya shughuli za ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama wa 2023, Mahakama iliandaa kongamano maalumu kuhusu mazungumzo baina ya vizazi kuhusu kazi ya Mahakama kwa lengo la kuanzisha urithi wa Mahakama kwa kuangalia mbele kwa kuhamasisha kada ya vijana kushika hatamu ya kueneza na kulinda haki za binadamu barani Afrika. Kutokan a na hili, wanafunzi wa shule za sheria barani Afrika, hasa wale wanaohusika katika kozi za shahada ya kwanza na uzamili zinazohusiana na kazi ya Mahakama, wawakilishi vikundi vya vijana vya vyama vya sheria au vyama vya wanasheria barani Afrika na wanasheia vijana wanaopenda kufanya utafiti kuhusu mfumo wa haki za binadamu wa Kiafrika walishiriki katika mazungumzo haya. Kwa ujumla, watu mia mbili (200), walishiriki ana kwa ana wakati mia mbili ishirini na watatu (223) walishiriki mtandaoni.

### b. Vikao vilivyofanyika

18. Katika kipindi cha kuripoti, Mahakama ilifanya Vikao vinne (4) vya Kawaida kama ifuatavyo:

    i. Kikao cha Kawaida cha 68, kuanzia tarehe 20 Februari hadi 17 Machi 202, jijini Arusha, Tanzania;
    ii. Kikao cha Kawaida cha 69, kuanzia tarehe 12 Juni hadi tarehe 7 Julai 2023, jijini Arusha, Tanzania;
    iii. Kikao cha Kawaida cha 70, kuanzia tarehe 5 hadi 30 Septemba 2022, jijini Arusha, Tanzania; na
    iv. Kikao cha Kawaida cha 71, kuanzia tarehe 6 Novemba hadi 4 Desemba 2023, huko Algiers, Algeria.

### c. Usimamizi wa Kesi

19. Sehemu hii inaelezea kwa upana vipengele vya kusimamia kesi, na inajumuisha kukubali vyombo husika vinavyoathiri usimamizi wa kesi, kama vile Taratibu za Kimahakama za Ndani za Mahakama.

20. Katika kipindi kinachotahminiwa, Mahakama ilitoa maamuzi arobaini na nane (48) kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

| Aina ya uamuzi | Jumla |
|---|---|
| **1.** Hukumu (Tafsiri) | 1 |
| **2.** Hukumu (Uzingaiaji wa sheria na fidia) | 28 |
| **3.** Maagizo (Mabadiliko ya Kichwa cha Maombi) | 1 |
| **4.** Maagizo (Uingiliaji kati) | 2 |
| **5.** Maagizo (Kuunganisha kesi) | 2 |
| **6.** Maagizo (Kufunguliwa tena) | 2 |
| **7.** Hukumu (Mamlaka ya Kisheria na Ukubalifu) | 9 |
| **8.** Hukumu (Suluhu za muda) | 3 |
| **Jumla Kuu** | **48** |

21. **Jedwali la 3** hapa chini linaonyesha maamuzi yaliyotolewa na Mahakama kuanzia Januari hadi Desemba 2023.

**Jedwali la 3: Maamuzi yaliyotolewa na Mahakama kuanzia Januari – Desemba 2023**

| Na. | Maombi Na. | Mleta Maombi | Mjibu Maombi |
|---|---|---|---|
| **A. Hukumu kuhusu Uzingaiaji wa Sheria na Fidia** | | | |
| 1. | 003/2016 | John Lazaro | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 2. | 003/2019 | Thomas Mgira | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 3. | 005/2019 | Issiaka KEÏTA na Wengine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 4. | 007/2016 | Matoke Mwita na mwingine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 5. | 011/2016 | Chacha Wambura | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 6. | 011/2020 | Bob Chacha Wangwe na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 7. | 013/2021 | Symon Vuwa Kaunda na wengine 5 | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 8. | 014/2017 | Hassan Bundala Swaga | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 9. | 015/2017 | Reuben Juma | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 10. | 018/2017 | Yassini Rashid Maige | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 11. | 019/2020 | Baedan Dogbo Paul na Mwingine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 12. | 022/2018 | Youssouf Traore na wengine 9 | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 13. | 024/2020 | Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 14. | 027/2016 | Marwa Rugumba Kisiri | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 15. | 028/2016 | Shija Juma | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 16. | 031/2016 | Umalo Mussa | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 17. | 032/2016 | Hoja Mwendesha | Jamhuri ya Mali |
| 18. | 032/2017 | Amos K | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 19. | 033/2016 | Makungu Misalaba | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20. | 037/2016 | Jackson Godwin | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 21. | 039/2020 | Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 22. | 041/2016 | La LIDHO, LE MIDH, LA FIDH na wengine | Jamhuri ya Cote d 'Ivoire |
| | | | |
| 23. | 045/2016 | Charo Said Kimilu na mwingine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 24. | 049/2016 | Chrizant John | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 25. | 057/2016 | Mulokozi Anatory | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 26. | 058/2016 | Niyonzima Augustine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **B. Hukumu kuhusu Tafsri** | | | |
| 27. | 004/2020 | Houngue Eric Noudehouenou | Jamhuri ya Benin |
| **C. Hukumu kuhusu Mamlaka ya Kisheria na Ukubalifu** | | | |
| 28. | 011/2021 | Lehady Vinagnon Soglo | Jamhuri ya Benin |
| 29. | 026/2017 | Mauridi Swedi@ Mswezi Kalijo | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 30. | 033/2017 | Leonard Moses | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 31. | 034/2016 | Juma Haruna | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 32. | 038/2019 | Amina Soumare | Jamhuri ya Mali |
| 33. | 054/2019 | Mama Seidou Samiratou | Jamhuri ya Benin |
| **D. Hukumu (Suluhu za Muda)** | | | |
| 34. | 001/2023 | Ayadhi Fathi na Wengine | Jamhuri ya Tunisia |
| 35. | 004/2023 | Moahd Kheriji Ghannouch na wengine | Jamhuri ya Tunisia |
| 36. | 009/2019 | Bahati Mtega na Mwingine | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **E. Maagizo (Kuunganisha Kesi)** | | | |
| 37. | 011/2016 | Chacha Wambura | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 38. | 015/2017 | Reuben Juma | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **F. Maagizo (Uingiliaji kati)** | | | |
| 39. | 006/2022 | Salaheddine Kchou | Jamhuri ya Tunisia |
| 40. | 010/2021 | Houngue Eric Noudehouenou | Jamhuri ya Benin |
| **G. Maagizo (Kufunguliwa tena)** | | | |
| 41. | 032/2016 | Hoja Mwendesha | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 42. | 051/2016 | Nzigiyimana Zabron | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **H. Maagizo (Mabadiliko ya Kichwa cha Maombi)** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 43. | 005/2019 | Issiaka KEÏTA na Wengine | Jamhuri ya Mali |

### d. Kupitisha Taratibu Mpya za Ndani za Kimahakama

22. Baada ya kupitisha Kanuni mpya za Mahakama mwaka 2020, Mahakama ilianza mapitio ya nyaraka nyingine za msingi za Mahakama zinazohusiana na usimamizi wa kesi, ili kuzilandanisha na Kanuni mpya. Katika Kikao chake cha Kawaida cha 71 kilichofanyika kuanzia Novemba 6 hadi Desemba 4, 2023 huko Algiers, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, mnamo Novemba 8, 2023, Mahakama ilipitisha Taratibu zake Mpya za Ndani za Kimahakama ambazo zilianza kutumika mara moja.

### e. Vikao vya Hadhara

23. Kuanzia tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba 2022, Mahakama iliandaa mikutano mitano (5) ya hadhara kuashiria ufunguzi rasmi wa mwaka wa mahakama na kutoa hukumu, amri, na maamuzi.

### f. Kutozingatia maamuzi ya Mahakama

*24.* Kwa mujibu wa Kifungu cha 31 cha Itifaki, katika kuwasilisha Ripoti yake ya Shughuli, Mahakama "… ripoti hiyo kwa umahususi, itabainisha kesi ambazo Serikali haijatii hukumu ya Mahakama". **Kiambatisho cha II** cha Ripoti hii kinaonyesha kesi ambazo Nchi hazijazingatia hukumu na maagizo ya Mahakama, baada ya tarehe ya mwisho iliyowekwa na Mahakama.

### g. Mpango wa Msaada wa Kisheria

25. Mahakama inasimamia Mpango wa Msaada wa Kisheria ambao unalenga kutoa msaada wa kisheria kwa waleta maombi masikini, na hivyo kuimarisha upatikanaji wa haki. Mnamo mwaka 2023, Mahakama ilishughulikia jumla ya maombi ishirini (20) ya msaada wa kisheria: waleta maombi wanane (8) walipewa msaada wa kisheria, kumi (10) hawakupewa msaada wa kisheria na wawili (2) walikuwa wanasubiri uamuzi wa Mahakama. Kati ya maombi 10 ambayo yalikataliwa, waleta maombi 4 walikuwa tayari wamewakilishwa na wakili na maombi yao yalikuwa yameandikiwa vizuri, wakati waleta maombi 6 walikuwa wameomba msaada wa kisheria ili kufuatilia kesi zao katika ngazi ya ndani, jambo ambalo Mahakama ya Afrika haina mamlaka ya kufanya hivyo.
26. Katika kipindi hicho hicho, Mahakama ilishughulikia maombi kumi na tisa (19) kutoka kwa wakili ambaye alitaka asajiliwe kwenye Orodha ya Mahakama. Maombi yalitoka kwa waleta maombi wanne (4) wa kike na kumi na tano (15) wa kiume kutoka: Burundi, Cameroon, Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ghana, Guinea, Kenya, Malawi, Niger, Nigeria, Rwanda, Senegal, Afrika Kusini, na Italia. Mahakama iliidhinisha maombi 14 ambayo yalitimiza vigezo vya wakili kuorodheshwa kwenye Orodha ya Mahakama kama ilivyoainishwa katika Sera ya Msaada wa Kisheria. Maombi matano yalikataliwa: waleta maombi 4 hawakuwa wamewasilisha hati zinazohitajika na 1 hakuwa na uzoefu wa miaka inayohitajika.

## B. Shughuli zisizo za kimahakama

27. Shughuli kuu zisizo za kimahakama zilizofanywa na Mahakama katika kipindi kinachotathminiwa zimeelezewa hapa chini:

### i. Kushiriki katika Mikutano ya Umoja wa Afrika

28. Mahakama ilishiriki katika Vikao vya Kawaida vya 44 na 45 vya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), Vikao vya Kawaida vya 42 na 43 vya Baraza la Utendaji, Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika. Mahakama pia ilishiriki katika Mkutano wa[5] wa Uratibu wa Nusu Mhula.

### ii. Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Utendaji

29. Katika Kikao chake cha Kawaida cha 41, kilichofanyika kuanzia tarehe 14 hadi 15 Julai 2022 huko Lusaka, Zambia, Baraza la Utendaji lilipitisha Uamuzi EX.CL/Des.**1177(XLI),** aya za 6 na 8 zilizoeleza kama ifuatavyo:

    ***6. INAOMBA*** *Tume na AfCHPR, ndani ya mfumo wa mageuzi ya kitaasisi yanayoendelea, kupendekeza haki na mafao mapya kwa Majaji wa AfCHPR.*

    ***8. INAOMBA*** *Tume na AfCHPR kuripoti kwa Baraza la Utendaji mnamo mwezi Februari 2023 kuhusu utekelezaji wa Uamuzi huu".*

30. Mnamo tarehe 14 Machi 2023, kando ya Kikao chake cha Kawaida cha 68, Mahakama ilifanya mkutano jijini Arusha, Tanzania, na Kitengo cha Mageuzi cha Tume ya Umoja wa Afrika (AUC) na Wataalamu kutoka Deloitte na Touche, walioajiriwa na AUC ndani ya mfumo wa Mageuzi ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika. Mahakama ilitoa mapendekezo ya mageuzi, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na muundo wake, akidi, kufutwa kwa Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, mfuko wa msaada wa kisheria wa Umoja wa Afrika, ufadhili wa Mahakama, malipo ya Majaji na marekebisho ya Rajisi ya Mahakama.

31. Kuanzia tarehe 8-11 Juni 2023, Mahakama ilihudhuria mapumziko ya pamoja huko Kigali, Rwanda kati ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) ya Umoja wa Afrika na Vyombo vya Umoja wa Afrika, kuhusu mageuzi ya Umoja wa Afrika. Wataalamu wa mchakato wa mageuzi kutoka Deloitte na Touche waliwasilisha ripoti yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya mamlaka na muundo wa vyombo vya Umoja wa Afrika. Kwa kujibu mapendekezo ya wataalamu, Mahakama ilitoa pendekezo la kuwa na mkutano wa mtandaoni na wataalamu pamoja na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamati ya Wataalamu wa Haki na Ustawi wa Mtoto, ili kujadili mapendekezo yanayohusiana na vyombo vya haki za binadamu vya Umoja wa Afrika.

32. Mnamo tarehe 20 Juni 2023, Mahakama, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamati ya Wataalamu wa Haki na Ustawi wa Mtoto

walifanya mkutano wa mtandaoni na Wataalamu kutoka Deloitte na Touche kuhusu mageuzi ya vyombo vitatu vya haki za binadamu vya Umoja wa Afrika. Katika suala hili, vyombo vitatu vya haki za binadamu vilisisitiza hitaji la mamlaka yao kubaki *jinsi yalivyo*. Vyombo hivyo vitatu baadaye viliwasilisha kwa Wataalamu hao mapendekezo yao tofauti ya mageuzi.

33. Baada ya mashauriano zaidi kuhusu Mageuzi ya vyombo hivyo, Mahakama, wakati wa Kikao chake cha 70 cha Kawaida kilichofanyika mnamo Septemba 2023, ilizingatia Uamuzi wa Baraza la Utendaji EX.CL/Des. 1177(XLI), hasa, aya ya 6, na kuandaa majibu yake, na kuyapeleka kwenye Kabineti ya Naibu Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika. Pendekezo hilo, kwa kiasi kikubwa linahusu kwamba mafao ya Majaji wa Mahakama ya Afrika, hayapaswi kubadilika, angalau kwa sasa.

**iii. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022**

34. Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mahakama kwa mwaka 2023 ilikuwa Dola za Marekani 11,982,334 ikiwa ni pamoja na Dola za Marekani 10,300,324 [asilimia 86] kutoka Nchi Wanachama na Dola za Marekani 1,682,010 [asilimia 14] kutoka kwa Washirika wa Kimataifa. Jumla ya utekelezaji wa bajeti kufikia mwishoni mwa tarehe 31 Desemba 2023 ilikuwa Dola za Marekani 11,100,622, ambayo inawakilisha kiwango cha utekelezaji wa bajeti cha asilimia 93. Kufikia tarehe 31 Desemba 2023, Mahakama ilikuwa imepokea michango kotoka katika nchi wanachama kwa mwaka 2023 (kwa robo 4) kiasi cha Dola za Marekani10,300,235 kutoka Nchi Wanachama na Dola za Marekani 737,858 kutoka kwa Washirika.

**iv. Ukuzaji uwezo na shughuli za uhamasishaji**

35. Mahakama ilifanya shughuli kadhaa za kukuza uwezo na uhamasishaji, zinazolenga kuongeza uwezo wa wafanyikazi na kuongeza uelewa miongoni mwa wadau, kuhusu uwepo wake na shughuli zake. Shughuli zilizofanywa ni pamoja na, *pamoja na nyingine,* mafunzo kwa wafanyakazi, ziara za uhamasishaji, mapumziko na mijadala, pamoja na mikutano iliyoandaliwa na wadau wengine muhimu.

**a. Maendeleo ya Uwezo wa Wafanyakazi**

36. Mahakama iliandaa shughuli zifuatazo, kati ya mambo mengine, zilizolenga kukuza uwezo wa wafanyakazi.

| **Orodha ya shughuli za kukuza uwezo zilizofanywa na Mahakama mwaka 2023** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Tarehe** | **Shughuli** | **Mahali** | **Mwandaaji** |
| **1** | Tarehe 10-14 Julai | Usimamizi wa Kumbukumbu za Kielektroniki za Mahakama | Dar es Salaam, Tanzania | Mahakama ya Afrika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2** | Tarehe 19-21 Septemba | Kongamano la Utoaji wa Huduma za Maktaba na Habari | Mwanza, Tanzania | Mahakama ya Afrika |
| **3** | Tarehe 09-13 Oktoba | Mafunzo ya Ngazi ya Juu ya Usimamizi wa Kimkakati | Johannesburg , Afrika Kusini | Mahakama ya Afrika |
| **4** | Tarehe 2 – 6 Oktoba | Usalama na ulinzi kazini | Arusha, Tanzania | Mahakama ya Afrika |
| **5** | Julai - Desemba | Mafunzo ya mtandaoni ya ALC – programu tumizi | Mtandaoni | Mahakama ya Afrika |
| **6** | Tarehe 28 Agosti hadi tarehe 1 Septemba 2023 | Uzinduzi wa SAP OpenText Utendaji kwa Mwafrika | Arusha, Tanzania | Mahakama ya Afrika |
| **7** | Tarehe 11-12 Novemba 2023 | Mafunzo ya Uongozi kwa Wafanyakazi wa Usimamizi | Arusha, Tanzania | Mahakama ya Afrika |

**ii. Ziara za uhamasishaji**

37. Katika kipindi kinachotathminiwa, Mahakama ilifanya ziara tano za uhamasishaji ili kushirikiana na Mataifa kuhusu kazi ya Mahakama kwa ujumla, na kuhimiza wale ambao hawajafanya hivyo, kuridhia Itifaki na/au kuweka Azimio la Kifungu cha 34(6).

**a. Ziara ya uhamasisjaji nchini Kenya**

38. Mahakama ilifanya ziara ya uhamasishaji nchini Jamhuri ya Kenya kuanzia tarehe 16 hadi tarehe 18 Julai 2023, kuhimiza nchi, ambayo tayari imeridhia Itifaki, iweke Azimio lililotajwa chini ya Kifungu cha 34(6).

39. Ujumbe wa Mahakama, ukiongozwa na Rais wake, ulikutana na kufanya majadiliano mazuri na maafisa wakuu wa serikali kutoka Serikali ya Kenya, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais, Dr. William Ruto, Rais wa Kenya, Waziri wa Mambo ya Nje, Mwanasheria Mkuu na Naibu Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Kenya. Ujumbe wa Mahakama ulitoa wito kwa mamlaka ya Kenya ichukue hatua za haraka kutekeleza hukumu ya Mahakama katika kesi ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Jamhuri ya Kenya.[1]

[1] Maombi 006/2012.

40. Mamlaka ya Kenya iliahidi kuzingatia maombi yaliyotolewa na Mahakama, na kuonyesha nia ya kushirikiana na wadau wote husika ili kuona namna bora ya kutekelezaHukumu hiyo.

**b. Ziara ya uhamasishaji nchini Msumbiji**

41. Mahakama ilifanya ziara ya uhamasishaji nchini Jamhuri ya Msumbiji kuanzia tarehe 9 hadi 11 Agosti 2023, ili kuihimiza nchi hiyo iweke Azimio kwa mujibu wa Kifungu cha 34(6).

42. Ujumbe wa Mahakama, ukiongozwa na Rais wake, ulikutana na kufanya majadiliano yenye tija na maafisa wakuu wa serikali wa nchi hiyo, ikiwa ni pamoja na, Mheshimiwa Rais, Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Waziri wa Sheria, Katiba na Masuala ya Kidini, Spika wa Bunge, Makamu wa Rais wa Mahakama Kuu, Naibu Mwanasheria Mkuu, Mchunguzi Maalumu, Mkuu wa Chama cha Wanasheria, Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu, Mkurugenzi wa Kitaifa wa Magereza.

43. Wakati wa ziara hiyo, Mahakama iliandaa Semina ya nusu siku kuhusu kazi ya Mahakama. Ili kukuza ushirikiano wake wa kitaasisi, Mahakama pia ilipendekeza kutia saini Mkataba wa Makubaliano (MOU) kati yake na Mahakama Kuu ya Msumbiji. Makubaliano haya yalisainiwa kando ya Majadiliano ya[6] ya Mahakama ya Umoja wa Afrika ambayo yalifanyika Algiers, Algeria mnamo Novemba 2023.

44. Mamlaka iliahidi kushauriana na wadau wote husika kabla ya kuamua kuhusu kuweka Azimio.

**c. Ziara ya uhamasishaji nchini Sao Tomé na Principe**

45. Mahakama ilifanya ziara ya uhamasishaji katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Sao Tomé na Principe kuanzia tarehe 10 hadi 12 Oktoba 2023 kuhamasisha nchi hiyo iridhie Itifaki na kuweka Azimio kulingana na Kifungu cha 34(6).

46. Ujumbe wa Mahakama, ukiongozwa na Rais wake, ulikutana na kufanya majadiliano yaliyozaa matunda na maafisa wakuu wa serikali wa nchi hiyo, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais Carlos Manuel Vila Nova, Rais wa wa Jamhuri ya Sao Tome na Principe, Waziri wa Sheria, Utawala wa Umma na Haki za Binadamu, Rais wa Mahakama Kuu, Rais wa Mahakama ya Katiba.

47. Wakati wa ziara hiyo, Mahakama iliandaa Semina ya nusu siku kuhusu kazi ya Mahakama. Ili kukuza ushirikiano wake wa kitaasisi, Mahakama pia ilipendekeza kutia saini Mkataba wa Makubaliano (MOU) kati yake na Mahakama Kuu ya Sao Tomé na Principe. Makubaliano haya yalisainiwa kando ya Majadiliano ya[6] ya Mahakama ya Umoja wa Afrika ambayo yalifanyika Algiers, Algeria mnamo Novemba 2023.

48. Mamlaka ilionyesha kuwa itafanya mashauriano zaidi na wadau wote husika nchini ili kuamua juu ya kuridhiwa kwa Itifaki na kuweka Azimio.

**d. Ziara ya uhamasishaji nchini Cape Verde**

49. Mahakama ilifanya ziara ya uhamasishaji katika Jamhuri ya Cape Verde kuanzia tarehe 16 hadi 18 Oktoba 2023 kuhamasisha nchi hiyo iridhie Itifaki na kuweka Azimio kulingana na Kifungu cha 34(6).

50. Ujumbe wa Mahakama, ukiongozwa na Rais wake, ulikutana na kufanya majadiliano yaliyozaa matunda na maafisa wakuu wa serikali wa nchi hiyo, ikiwa ni pamoja na, heshimiwa Rais José Maria Neves ,Rais wa Cape Verde, Waziri wa Sheria, Katibu wa Nchi, Mambo ya Nje, Rais wa Mahakama Kuu, Mwanasheria Mkuu, Rais wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu, Rais wa Baraza Kuu la Mahakama.

51. Wakati wa ziara hiyo, Mahakama iliandaa Semina ya nusu siku kuhusu kazi ya Mahakama. Ili kukuza ushirikiano wake wa kitaasisi, Mahakama pia ilitia saini Mkataba wa Makubaliano (MOU) na Mahakama Kuu ya Cape Verde. Makubaliano haya yalisainiwa kando ya Majadiliano ya[6] ya Mahakama ya Umoja wa Afrika ambayo yalifanyika Algiers, Algeria mnamo Novemba 2023.

Mamlaka iliahidi kushauriana na wadau wote husika nchini ili kuridhia Itifaki na kuweka Azimio.

**e. Ziara ya uhamasishaji nchini Algeria**

52. Wakati wa Kikao cha Kawaida cha 71 cha Mahakama kilichofanyika Algiers, Algeria kuanzia tarehe 6 Novemba hadi 4 Desemba, Mahakama ilichukua fursa ya kufanya ziara za heshima na kufanya majadiliano yaliyozaa matunda na maafisa wa ngazi ya juu wa serikali nchini humo, pamoja na mambo mengine, kuwaeleza kuhusu kazi ya Mahakama, na kuhimiza Algeria, ambayo iliridhia Itifaki ya kuanzisha Mahakama mnamo 2003, ifikirie kuweka Azimio linalotakiwa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki.

53. Kuanzia tarehe 26 Novemba hadi tarehe 4 Desemba 2023, ujumbe wa Mahakama ulimtembelea Mheshimiwa Rais, Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Nchi, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Sheria, Rais wa Seneti, Rais wa Mahakama Kuu, Rais wa Baraza la Katiba, Baraza la Kitaifa la Haki za Binadamu na Chama cha Wanasheria wa Algeria. Mahakama ilipokea hakikisho kutoka kwa mamlaka kwamba serikali ilikuwa inazingatia ombi hilo.

**iii. Mapumziko ya Majaji wa Mahakama ya Afrika**

54. Mahakama ya Afrika ilikwenda katika Mapumziko yake ya Pili ya Majaji kuanzia tarehe 14 hadi 16 Juni 2023 huko Dodoma, Tanzania. Mapumziko hayo, ambayo yalihudhuriwa na Majaji na Wafanyakazi wa Rajisi wa Mahakama, yalikuwa ni ufuatiliaji wa mapumziko ya kwanza yaliyofanyika tarehe 2 na 3 Juni 2021 jijini Arusha, Tanzania.

55. Lengo la Mapumziko lilikuwa kuangalia njia za ufanyaji kazi za Mahakama kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa Mahakama katika kulinda haki za binadamu barani.

56. Mahakama ilipitisha Azimio la Dodoma ambalo lilitoa miongozo ya wazi, pamoja na mengine, kuhusu jukumu la Mwandishi wa Majaji katika kukamilisha

hukumu, jinsi ya kutekeleza kwa ufanisi Mpango wa Ukamilishanaji kati ya Mahakama ya Afrika na Tume ya Afrika, jinsi ya kuimarisha utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama, maandalizi ya maoni ya Majaji, utoaji wa fidia, na matumizi ya kanuni ya kiasi cha shukrani.

**iv. Mapumziko ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kuhusu Mageuzi ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika**

57. Kuanzia tarehe 8-11 Juni 2023, Mahakama ilihudhuria mapumziko ya pamoja huko Kigali, Rwanda kati ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) ya Umoja wa Afrika na Vyombo vya Umoja wa Afrika, kuhusu mageuzi ya Umoja wa Afrika. Wataalamu wa mchakato wa mageuzi waliwasilisha ripoti yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya mamlaka na muundo wa vyombo na taasisi za Umoja wa Afrika. Kwa kujibu mapendekezo ya wataalamu, Mahakama ilitoa pendekezo la kuwa na mkutano wa mtandaoni na wataalamu pamoja na Tume ya Afrika na Kamati ya Wataalamu wa Haki za Mtoto, ili kujadili mapendekezo yanayohusiana na vyombo vya haki za binadamu vya Umoja wa Afrika.

**v. Kushiriki katika uandaaji wa Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika**

58. Kuanzia tarehe 2-5 Agosti 2023, Mahakama ilihudhuria mkutano wa wataalamu wa kiufundi kuhusu maendeleo ya Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika 2024-2028 ambao ulifanyika Midrand, Afrika Kusini. Wakati wa mkutano huu wataalamu walikamilisha kuweka mwelekeo thabiti wa Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika wa mwaka 2024-2028 na kuweka fremu ya Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika wa mwaka 2024-2028. Aidha, Mahakama ilihudhuria kwenye mkutano huko Lusaka, Zambia uliohusu mada hiyo hiyo ili kuandaa uchanganuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vitishio (SWOT) kwa ajili ya Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika wa mwaka (2024-2028), na kuboresha malengo muhimu ya Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika (2024-2028). Mikutano ya mtandaoni pia ilifanyika tarehe 14 na 20 Septemba 2023, ambapo wataalamu waliandaa Mfumo wa Kutathmini Malengo ya Mkakati wa umoja wa Afrika na Mahakama ilichangia katika mikutano yote miwili.

59. Kuanzia tarehe 2 – 6 Oktoba 2023, Mahakama ilihudhuria mkutano wa wataalam kuhusu Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika wa mwaka 2024-2028 huko Kigali, Rwanda kuhusu mapitio na kurekebisha Mfumo wa Tathmini wa Mkakati wa Umoja wa Afrika. Lengo la Mahakama lilikuwa kwenye Lengo Kuu la 3 - *"Taasisi za umma zinazingatia zaidi mahitaji ya raia*" ambapo, Mahakama ilichangia katika uundaji wa malengo maalumu ya kimkakati ya haki za binadamu. Mfumo wa Tathimi ya Malengo ya Makakati uliorekebishwa vizuri uliwasilishwa kwa Wakurugenzi wa vyombo vya Umoja wa Afrika ambao walikagua hati hiyo na kutoa maoni.

**vi. Mapumziko ya Baraza la Utendaji ya Umoja wa Afrika kuhusu Ajenda 2063**

60. Kuanzia tarehe 1 hadi tarehe 3 Oktoba 2023, Mahakama ilihudhuria Mkutano wa Baraza la Utendaji la Umoja wa Afrika kuhusu Ajenda 2063, uliofanyika Kigali, Rwanda. Mapumziko hayo yalichunguza kiwango cha

utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063, na pia kuangalia rasimu ya Mpango wa Pili wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063.

61. Wakati wa Mapumziko, Rais wa Mahakama alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuhakikisha haki za binadamu zinaingizwa kikamilifu katika Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi.

#### vii. Majadiliano ya 6 ya Mahakama ya Umoja wa Afrika

62. Chini ya usimamizi wa Umoja wa Afrika (AU), Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, iliandaa Majadiliano ya Sita ya Mahakama ya Umoja wa Afrika yaliyokuwa na mada ya: *"Kuendeleza Haki za Binadamu barani Afrika: Changamoto na fursa za kuunganisha sheria za haki za binadamu za kikanda na kimataifa katika mahakama za ndani",* kuanzia tarehe 20 hadi 22 Novemba 2023, huko Algiers, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria.

63. Mazungumzo ya Mahakama yalifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Nadir Larbaoui, Waziri Mkuu, aliyewakilishwa na Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria.

64. Lengo kuu la Majadiliano ya Sita ya Mahakama ya Umoja wa Afrika lilikuwa kutoa jukwaa kwa ajili ya majaji wa mahakama za kitaifa na kikanda na wadau wengine ili kujadili changamoto na fursa zinazohusiana na kuunganisha sheria za haki za binadamu za kikanda na kimataifa katika mahakama za ndani barani Afrika. Pia ililenga kuchunguza, kujadili, na kuchambua utekelezekaji wa Itifaki ya Maputo, mwenendo unaobadilika wa haki za binadamu kuhusu haki za wanawake ndani ya mfumo wa haki za binadamu wa Afrika, na umuhimu mkubwa wa kujenga uelewa kati ya Majaji Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, kuhusu umuhimu wa ujumuishaji wa utambuzi huu katika mifumo yao ya kisheria ya ndani. Mazungumzo pia yaliwapa washiriki fursa ya kujadili na kushiriki uzoefu kuhusu mwenendo wa kisheria kutokana na kesi inayohusu uhalali wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

65. Taarifa ya Mwisho ya Majadiliano ya 6 ya Mahakama ya Umoja wa Afrika , ambayo inaelezea matokeo makuu ya Majadiliano, imeambatishwa katika Ripoti hii kama **Kiambatisho cha III.**

### C. Mipango mingine ya utandaaji na kujenga mitandao

#### i. Kushirikiana na wadau wengine

66. Mahakama ilifanya shughuli kadhaa, pamoja na mambo mengine, zilizoleanga kuongeza uelewa kati ya wadau, kuhusu uwepo wake na shughuli zake kulingana na malengo yake katika Mpango Mkakati wa 2021-2025. Kuhusiana na jambo hili, Rais, Majaji na watumishi waandamizi wa Mahakama walikuwa wakishiriki katika shughuli kadhaa za utandaaji zilizoandaliwa na wadau wengine husika, zenye lengo la kufanya Mahakama ijulikane zaidi. Shughuli hizi, zilijumuisha zifuatazo:

| Na | **Tarehe** | **Shughuli** | **Mahali** | **Mwandaaji** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tarehe 2-3 Machi 2023 | Jukwaa kuhusu Utu na Maendeleo | Indiana Chicago | Chuo Kikuu cha Notre Dame |
| 2 | Tarehe 11-14 Mei 2023 | Mkutano wa Biennial wa Majaji Wanawake | Marrakesh Moroko | IAWJ |
| 3 | Tarehe 20-21 Julai 2023 | Kongamano la Sheria Duniani | Jiji la New York | Msingi wa Sheria wa Mwanasheria Duniani |
| 4 | Katikati ya Septemba | Mkutano wa Kimataifa kuhusu Sheria ya Katiba | Marrakech | Chuo Kikuu cha Charles Jamhuri ya Cheki |
| 5 | Tarehe 19 Oktoba 2023 | Maadhimisho ya miaka 20 ya Itifaki ya Maputo | Arusha | Taasisi ya Sheria ya Kimataifa ya Afrika (AIIL) |
| 6 | Tarehe 22-27 Oktoba 2023 | Mkutano wa Jukwaa la Majaji Wakuu wa Kusini na Mashariki mwa Afrika na Mkutano Mkuu wa Mwaka | Arusha | Jaji Mkuu wa Tanzania |
| 7 | Tarehe 24 Oktoba 2023 | Majadiliano ya Wadau kuhusu kuridhia Itifaki ya Mahakama ya Afrika | Arusha | Kituo cha Haki za Binadamu Pretoria na Muungano wa Mahakama ya Afrika |
| 8 | Tarehe 21-22 Oktoba 2023 | Kongamano la Amani na Usalama la Lomé | Lomé, Togo | MOFA Togo |
| 9 | Tarehe 21-27 Oktoba 2023 | Ziara ya heshima ya kikosi kazi ili kuimarisha ushirikiano | Arusha | Mwandishi maalumu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa |
| 10 | Tarehe 2-3 Novemba 2023 | Mwaliko kuhudhuria Toleo la 28 la Kongamano la Kimataifa, | New York | Chama cha Wanasheria Duniani (WJA) |
| 11 | Tarehe 2-3 Novemba 2023 | Maadhimisho ya kimataifa ya siku ya kimataifa ya kukomesha ukosefu wa adhabu kwa uhalifu unaofanywa dhidi ya waandishi wa habari | Washington D.C | Mwandishi maalumu wa uhuru wa kujieleza (IACHR/RELE) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12 | Tarehe 4-5 Desemba 2023 | Mwaliko wa Kikao cha Wazi cha Mawaziri na cha Ngazi ya Juu kuhusu Kukuza na Kulinda Haki na Ustawi wa Watoto walio Katika Mazingira ya Migogoro Barani Afrika | Gambia | Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika |
| 13 | Tarehe 9 Desemba 2023 | Uzinduzi wa chakula cha jioni cha kila mwaka cha Mtandao wa Mawakili Wanawake (FLN) | Kampala Uganda | Mtandao wa Wanasheria wanawake (Uganda) |
| 14 | Tarehe 11-12 Desemba 2023 | Kushiriki katika Tukio Kubwa la "Haki za Binadamu 75" | Geneva | Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa |

### ii. Uhusiano na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

67. Mahakama na Tume ya Afrika zinaendelea kuimarisha uhusiano wao na kuimarisha ukamilishanaji unaotarajiwa kulingana na Itifaki. Mahakama ilishiriki katika sherehe za ufunguzi wa Vikao vya Kawaida vya 76 na 77 vya Tume ya Afrika. Mikutano hii ilichangia kuimarisha uhusiano kati ya vyombo hivyo viwili.

### iii. Mahusiano na Wanachama Wataalamu wa Utawala wa Afrika

68. Mahakama ilifanya kazi kwa karibu na Jukwaa la Wataalamu wa Utawala wa Afrika (AGA) na ilishiriki katika mikutano ya kiufundi na ya kikanuni na matukio mengine yaliyoandaliwa na Jukwaa hilo. Ilishiriki kikamilifu katika mikutano mbalimbali iliyofanyika mwaka mzima na ilibaini maeneo ambayo ushirikiano wa karibu unapaswa kuendelezwa na washiriki mbalimbali wa jukwaa la AGA, hasa kuhusiana na uandaaji wa shughuli za pamoja.

69. Mnamo tarehe 13 na 14 Januari 2023, Rajisi ya Mahakama ilishiriki katika mkutano wa mtandaoni kwa ajili ya kupitia na kuthibitisha Ripoti ya Utawala wa Afrika (AGR-23) na ikatoa maoni na mazingatio yake. Wakati wa kikao cha kikanuni mnamo tarehe 13 Februari ikifuatiwa na mkutano wa kisiasa mnamo tarehe 14 Februari, ujumbe wa mahakama ulipendekeza shughuli za pamoja zitakazotekelezwa na washiriki wa Jukwaa hilo.

70. Katika mapumziko ya kimkakati, yakifuatiwa na mkutano wa kisiasa kuanzia tarehe 6 hadi 12 Julai, 2023 uliofanyika jijini Nairobi Kenya, Rajisi ya Mahakama ilitathmini mpango makakati wa jukwaa wa 20206-2023 ambao ulitathminiwa na kupitishwa. Rajisi ya Mahakama pia ilitathmini ripoti za awali za Togo na Rwanda kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Utawala, Demokrasia na Uchaguzi na iliwasilisha mazingatio na mapendekezo yake. Warsha za vijana na wanawake kama watendaji katika sera ya biashara huria ya Afrika zilitoa fursa kwa Rajisi ya Mahakama kutoa masuluhisho na mapendekezo kwa ajili ya urahisi wa kufanya biashara miongoni mwa nchi za Afrika.

71. Mahakama inaendelea kufanya kazi na wadau husika, ikiwa ni pamoja na washirika wa nje, kwa ajili ya kuendeleza mpango wa AGA-SP, awamu ya kwanza inaelekea kukamilika. Kuhusiana na hili, Rajisi ilishiriki katika mkutano

wa tathmini ya mradi uliofanyika Johannesburg mnamo tarehe 12 na 13 Juni 2023.

### iv. Kushiriki katika Jukwaa la Tatu la Kimataifa la Haki za Binadamu

72. Ujumbe wa Mahakama ya Afrika, ukijumuisha Majaji na wafanyakazi wa Rajisi, ulishiriki katika Jukwaa la[3] la Kimataifa la Haki za Binadamu (Jukwaa) ambalo liliandaliwa na Mahakama ya Haki za Binadamu ya Marekani (Mahakama ya Marekani) kuanzia tarehe 25 hadi 26 Mei 2023. Kongamano hilo lilifanyika katika Makao Makuu ya Mahakama ya Bara la Amerika huko San Jose, Costa Rica. Mahakama zote tatu za kikanda za haki za binadamu, yaani, Mahakama ya Afrika, Mahakama ya Bara la Amerika na Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu ziliwakilishwa katika Kongamano hilo.

73. Kongamano hilo liliandaliwa kama mazungumzo kati ya mahakama tatu za haki za binadamu za kikanda na majadiliano yalifanyika kwa kuangazia vizuizi viwili vikuu. Sehemu ya kwanza ilihusu 'uhuru wa mahakama na utawala wa sheria' wakati sehemu ya pili ililenga 'mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na haki za binadamu.' Jukwaa hili pia lilijumuisha utoaji wa Semina katika Chuo Kikuu cha Costa Rica iliyohusu 'Mifumo ya kikanda ya kulinda haki za binadamu na changamoto zake.'

74. Mwishoni mwa Kongamano, Mahakama hizo tatu zilipitisha Azimio, Azimio la San Jose, ambalo pamoja na mambo mengine, lilisisitiza kwamba demokrasia, utawala bora na ufikiaji mzuri wa haki na uhuru wa mahakama ni muhimu kwa ulinzi na utambuzi wa haki za binadamu na demokrasia bora. Azimio hilo pia lilitambua umuhimu wa kuimarisha uratibu na ushirikiano kati ya mahakama za kikanda na kusisitiza kujizatiti kwa Mahakama hizo tatu katika kuchangia mazungumzo ya kudumu na njia za mashauriano kati yao.

75. Azimio hilo pia liliamuru uhuishaji wa Mkataba wa Makubaliano ya Sehemu Tatu kwa miaka minne ambao ulisainiwa mnamo Oktoba 2019 mwishoni mwa Kongamano la Kwanza la Kimataifa la Haki za Binadamu ambalo lilifanyika Kampala, Uganda.

76. Mnamo tarehe 27 Novemba 2023, Mahakama hizo tatu zilichapisha Juzuu ya 3 ya Ripoti yao ya Sheria ya Pamoja, kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano. Ripoti hii ya Sheria inafuata muundo sawa na ule wa awali, uliogawanywa katika sura tatu, moja kwa kila Mahakama. Kila sura inaangazia kesi kuu ambazo zinawakilisha viwango vipya au maendeleo ya kibunifu ya sheria katika kipindi cha mwaka, 2021. Mchango wa Mahakama ya Afrika kwenye Toleo la Tatu la Ripoti ya Sheria ya Mahakama hizo Tatu unajumuisha kesi tatu, zinazohusiana na: kutotekeleza hukumu ya awali; mamlaka binafsi na kukamilisha taratibu za ndani.

### v. Mazungumzo na Mahakama za Kanda Ndogo

77. Mahakama inaendelea kukuza uhusiano thabiti na mahakama za kanda ndogo barani. Kuanzia tarehe 22 hadi 24 Juni 2023, Mahakama ya Jumuiya, ECOWAS (Mahakama ya ECOWAS) na Mahakama ya Afrika zilifanya Mazungumzo ya Pili ya Kimahakama kati ya Mahakama hizo mbili jijini Arusha, Tanzania. Majaji wote wa Mahakama zote mbili walihudhuria kwenye Mazungumzo hayo na walikuwa wakiongozwa na Rais wa Mahakama ya Afrika, Mheshimiwa Jaji Imani D. Aboud na Rais wa Mahakama ya ECOWAS, Mheshimiwa Jaji Edward Amoako Asante.

78. Majadiliano ya miaka miwili yalilenga kuimarisha uhusiano kati ya Mahakama hizo mbili katika kulinda haki za binadamu na watu na kutathmini utekelezaji wa Hati ya Makubaliano (MOU) iliyotiwa saini na pande zote mbili mnamo tarehe 1 Machi 2018. Mahakama hizo mbili zilihuisha Hati ya Makubaliani kwa kipindi kingine cha miaka mitano, kuanzia tarehe 24 Juni 2023.

79. Chini ya Hati Mpya ya Makubaliano, Mahakama hizo mbili zimejizatiti kuimarisha uhusiano wao mzuri uliopo na kwa lengo hili, zimekubaliana kuhusu mipango kadhaa ya kuboresha utekelezaji wa mamlaka zao husika. Maeneo ya ushirikiano yaliyotambuliwa ni pamoja na kubadilishana wafanyakazi, uwakilishi, mafunzo ya pamoja, maarifa na kubadilishana taarifa, uchapishaji wa taarifa za mwenendo wa kisheria, utafiti na kujenga uwezo ndani ya mfumo wa vyombo vinavyounda Mahakama hizo mbili. Mahakama hizo mbili pia zilipitisha Mpango Kazi wa miaka mitano.

80. Mnamo tarehe 20 Septemba 2023, Majaji wa Mahakama ya Afrika na Majaji wa Mahakama ya Umoja wa Kiuchumi na Fedha wa Afrika Magharibi (Mahakama ya WAEMU) walifanya Mazungumzo ya Pili ya Kimahakama kati ya Mahakama hizo mbili jijini Arusha, Tanzania. Mazungumzo hayo yaliongozwa na Rais wa Mahakama ya Afrika, Mheshimiwa Jaji Imani D. ABOUD, na Rais wa Mahakama ya WAEMU, Mheshimiwa Jaji Mahawa Sémou DIOUF.

81. Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha uhusiano kati ya Mahakama hizo mbili katika kulinda haki za binadamu na watu na kuchunguza fursa na matarajio ya ushirikiano wa kimahakama. Mahakama hizo mbili zilitia saini Mkataba wa Makubaliano wa miaka mitano, unaoanza kutumika kuanzia tarehe 20 Septemba 2023.

vi. **Mahusiano na Washirika**

82. Mahakama inaendelea kunufaika na msaada wa washirika wake wa siku zote, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, (OHCHR), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani GMZ (GIZ). Washirika hawa wanaendelea kusaidia shughuli za utaandaaji za Mahakama, ikiwa ni pamoja na ziara za uhamasishaji, majadiliano na mahakama za kitaifa, za kikanda na kimataifa, na ukuzaji wa uwezo wa kitaasisi.

**Makubaliano ya Wenyeji na uhusiano na Nchi Mwenyeji**

83. Mahakama inaendelea kufanya kazi na Nchi Mwenyeji, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kutekeleza kwa ufanisi Mkataba wa Uenyeji. Iliimarisha ushirikiano wake na mamlaka ya Nchi Mwenyeji mwaka 2023, pamoja na mambo mengine, ili kuhimiza Tanzania, kutafakari upya kuweka Azimio la Kifungu cha 34(6), na pia kujenga majengo ya kudumu ya Mahakama. Ili kufikia lengo hili, Rais wa Mahakama alikutana na kufanya majadiliano mazuri na Waziri wa Mambo ya Nje na Waziri wa Katiba mnamo mwezi Januari 2023; naye pia aliwahutubia Majaji jijini Arusha mnamo mwezi Februari 2023, na Juni 2023, ujumbe wa Mahakama ulimtembelea Waziri wa Mambo ya Nje katika mji mkuu wa Dodoma. Mnamo mwezi Juni 2023, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, ambayo inasimamia ujenzi wa majengo ya Mahakama ilitembelea

Mahakama na pia kukagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama.

84. Mnamo tarehe 2 Juni 2023, Nchi Mwenyeji ilizindua rasmi eneo la ujenzi wa makao makuu ya kudumu ya Mahakama, kwa kukabidhi rasmi eneo hilo kwa Kampuni ya Ujenzi katika sherehe iliyoongozwa na Katibu wa Kudumu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbele ya Rais na Makamu wa Rais wa Mahakama ya Afrika. Mnamo mwezi Agosti 2023, kazi ya kujenga majengo ilianza kwa bidii na serikali imeonyesha kuwa ujenzi huo utakamilika ndani ya kipindi cha kati ya miezi 18 na 24.

## V. TATHMINI NA MAPENDEKEZO

### iii. Tathmini

85. Tangu Mahakama ianze shughuli zake mwaka 2006, Mahakama imechangia katika kuendeleza sheria za haki za binadamu za Afrika na ulinzi wa haki za binadamu na watu barani humo. Mwenendo wa kisheria wa Mahakama unashughulikia maswala anuwai yanayounda mazingira ya kijamii na kiuchumi na kisiasa ya bara, pamoja na maswala ya uchaguzi, utawala bora, uhuru wa kujieleza, na haki za wazawa, n.k.

86. Kaulimbiu ya Mahakama ya mwaka 2023 ilikuwa "*kuunganisha mfumo wa mwenendo wa kisheria wa haki za binadamu wa kikanda na kimataifa katika mahakama za kitaifa*"***.*** Kaulimbiu hii si tu inafaa bali pia imekuja katika wakati mwafaka zaidi, kwani mwaka 2023 ni Maadhimisho ya Miaka 60 ya kupitishwa kwa Mkataba na hatimaye kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika. Mkataba wa Umoja wa Afrika (OAU) ulijumuisha ndoto ya waanzilishi wa OAU ya Afrika yenye umoja, nguvu na ustawi, na kwamba uhuru, usawa, haki, amani na utu vilikuwa muhimu katika kufanikisha ndoto hii.

87. Mnamo mwaka 2013, nusu karne baada ya kuanzishwa kwa OAU, katika kile kilichoitwa Mkutano wa Jubilee ya Dhahabu, viongozi wa Afrika walipitisha mpango mwingine, Ajenda 2063, kama msingi wa mabadiliko ya muda mrefu ya kijamii na kiuchumi na ujumuishaji barani Afrika.

88. Kwa hivyo, mada ya Mahakama ya mwaka 2023 kwa ililenga kuibua tena mjadala huu kuhusu kiini halisi, si tu kwa ajili ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika, lakini mfumo mzima wa haki za binadamu wa Afrika na muundo wa Umoja wa Afrika. Ilikuwa tafakari kuhusu jinsi haki za binadamu zinavyoweza na zinavyopaswa kuchangia katika kufanikisha malengo ya Umoja wa Afrika kwa ujumla na Matarajio ya Ajenda 2063 kwa umahususi.

89. Mahakama inaamini sana kwamba Afrika tunayotaka haiwezi kujengwa juu ya ujumuishaji wa kisiasa peke yake. Ni jambo linalowahitaji wapiga kura wote, ikiwa ni pamoja na utawala bora na kuheshimu haki za binadamu. Historia inatufundisha kwamba uchumi wowote thabiti na jamii thabiti kote ulimwenguni

zimejengwa juu ya msingi thabiti wa utawala wa sheria, haki na kuheshimu haki za binadamu. Kwa hivyo ni muhimu kwamba ikiwa Afrika inataka kuendelea, ikiwa Afrika inataka kufanikiwa, ikiwa Afrika inataka kuungana, ikiwa Afrika inataka kunyamazisha bunduki, na ikiwa kweli tunatamani AFRIKA TUNAYOTAKA, vitendo vyetu lazima viongozwe na haki, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu.

90. Mojawapo ya sababu kuu zinazozuia utekelezaji mzuri wa mamlaka ya Mahakama ni ushirikiano usiotosha kutoka kwa Nchi Wanachama. Hadi leo, zaidi ya miaka ishirini na mitano baada ya kupitishwa kwa Itifaki ya kuanzisha Mahakama, ni Nchi 34 tu kati ya nchi Wanachama 55 wa Umoja wa Afrika ambazo zimeridhia Itifaki hiyo. Kati ya Nchi 34 Wanachama, ni 8 tu ndizo zimeweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki. Aidha, kati ya maamuzi zaidi ya 200 yaliyopitishwa na Mahakama tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002, chini ya asilimia 10 yametekelezwa.

91. Licha ya changamoto hizi, Mahakama ya Afrika ina maoni kwamba jukumu la Nchi Wanachama katika ulinzi wa haki za binadamu halipaswi kupuuzwa. Ili kufikia lengo hili, Mahakama iliendelea na diplomasia yake ya mahakama na ujumbe wa uhamasishaji kwa Nchi Wanachama. Mnamo mwaka 2023, Mahakama ilitembelea nchi tano, Kenya, Cape Verde, Sao Tomé na Principe, Msumbiji na Algeria, ili kuwashirikisha katika majadiliano yaliyozaa matunda na ya kujenga kuhusu kazi ya Mahakama, na hitaji la aidha kuridhia Itifaki au kuweka Azimio au kufanya yote mawili, kulingana na hali itakavyokuwa.

92. Mahakama pia imetafuta ushirikiano na mahakama nyingine ndogo za haki za binadamu za kikanda na bara, kwa lengo la kuashiria, kushiriki uzoefu na mazoea bora katika eneo la haki za binadamu na usimamizi sahihi wa haki. Kwa hivyo Mahakama ilishiriki katika Kongamano la Tatu la Kimataifa la Haki za Binadamu huko Costa Rica na kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya ECOWAS na Mahakama ya Haki ya Umoja wa Kiuchumi na Fedha wa Afrika Magharibi. Toleo la 2023 la Majadiliano ya Kimahakama ya Umoja wa Afrika liliwaleta pamoja Majaji Wakuu na Marais wa Mahakama za Katiba kutoka Nchi 37 Wanachama wa Umoja wa Afrika kujadili ushirikiano kati ya mahakama za kitaifa na za kikanda katika kulinda haki za binadamu. Ushirikiano huu ulitoa fursa kwa Mahakama ya Afrika kuunda uhusiano wenye tijna na vyombo kama hivyo katika ngazi ya kitaifa, kikanda na bara kwa lengo la kuendeleza ulinzi wa haki za binadamu na usimamizi wa haki kwa ujumla.

93. Mahakama inatambua kwamba jukumu lake ni kukamilisha kazi ambayo Nchi Wanachama zinafanya katika ngazi ya ndani ili kukuza na kulinda haki za binadamu na watu. Mahakama haipaswi na haiwezi kuchukua nafasi ya taasisi za ndani zilizopewa kazi hii, kwani jukumu la msingi la kukuza na kulinda haki za binadamu ni la Nchi Wanachama.

94. Ili kufikia lengo hili, Mahakama imeamua kuimarisha ushirikiano wake na Nchi Wanachama mwaka 2024, ili kuhakikisha kuwa wanaelewa vya kutosha jukumu la Mahakama na jinsi Mahakama inavyofanya kazi.

### ii. Mapendekezo

95. Kulingana na yaliyotajwa hapo juu, Mahakama inawasilisha mapendekezo yafuatayo kwa ajili ya kuzingatiwa na kupitishwa na Baraza la Utendaji:

i. **Inatoa wito** kwa Nchi ishirini na moja (21) Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo bado hazijaingia kwenye Itifaki zifanye hivyo, ili kuhakikisha mamlaka ya Mahakama ya Afrika na inatambuliwa na Nchi zote hamsini na tano (55) za Umoja wa Afrika;
ii. **Inatoa wito** kwa Nchi ishirini na sita (26) Wanachama wa Itifaki ambazo bado hazijaweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) zifanye hivyo;
iii. **Inahimiza** Nchi Nne (4) Wanachama wa Itifaki ambazo ziliondoa Azimio lao la Kifungu cha 34(6) zitafakari upya uamuzi wao;
iv. **Inaomba** Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AUC) achukue hatua zote muhimu kuanzisha Mfuko wa Msaada wa Kisheria kwa ajili ya Vyombo vya Haki za Binadamu vya Umoja wa Afrika;
v. **Inawaalika** na kuhimiza Nchi zote Wanachama na wadau wengine wa haki za binadamu barani kutoa michango ya hiari ya ukarimu kwa ajili ya Mfuko wa Msaada wa Kisheria ili kuhakikisha uendelevu na mafanikio yake;
vi. **Inaomba** Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zishirikiane na Mahakama na kuzingatia maamuzi yake;

## KIAMBATISHO CHA I

## ORODHA YA MAJAJI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU KUFIKIA DESEMBA 31, 2022

| Na. | Jina | Mhula | | Nchi |
|---|---|---|---|---|
| | | Muda | Mwisho wa kutumikia | |
| 1 | Jaji Imani D. Aboud | 6 | 2026 | Tanzania |
| 2 | Jaji Modibo Sacko | 6 | 2026 | Mali |
| 3 | Jaji Ben Kioko | 6 | 2024 | Kenya |
| 4 | Jaji Rafaâ Ben Achour | 6 | 2026 | Tunisia |
| 5 | Jaji Ntyam Ondo Mengue | 6 | 2028 | Kameruni |
| 6 | Jaji Tujilane Rose Chizumila | 6 | 2029 | Malawi |
| 7 | Jaji Chafika Bensaoula | 6 | 2029 | Algeria |
| 8 | Jaji Blaise Tchikaya | 6 | 2024 | Kongo |
| 9 | Jaji Stella I. Anukam | 6 | 2024 | Nigeria |
| 10 | Jaji Dumisa Ntsebeza | 6 | 2026 | Afrika Kusini |
| 11 | Jaji Dennis D. Adjei | 6 | 2028 | Ghana |

| | | |
|---|---|---|
| **AFRICAN UNION** | | **UNION AFRICAINE** |
| **الاتحاد الأفريقي** | | **UNIÃO AFRICANA** |

**AFRICAN COURT ON HUMAN AND PEOPLES' RIGHTS**
**COUR AFRICAINE DES DROITS DE L'HOMME ET DES PEUPLES**

P.O Box 6274 Arusha, Tanzania Telephone: +255 732 979506/9; Fax: 255 732 979503
Web site: www.african-court.org / Email : registrar@african-court.org

# RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA HUKUMU ZILIZOTOLEWA NA MAHAKAMA 2023

**HALI KUFIKIA TAREHE 30 NOVEMBA 2023**

**KIAMBATISHO II**

## I. UTANGULIZI

1. Taarifa hii inahusu utekelezaji wa hukumu za Mahakama hii kufikia tarehe 30 Novemba 2023.

2. Kwa kuwa ripoti hii inahusu hasa hali ya utekelezaji wa hukumu za Mahakama hii, haitoi maoni yoyote juu ya hukumu ambazo Mahakama hii haijabaini ukiukwaji wowote wa sheria.

3. Kwa mujibu wa maelekezo ya Mahakama hii kupitia kikao cha 63, mashauri yamepangwa kwa alfabeti kulingana na Nchi Mjibu Maombi. Aidha, mashauri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo Mahakama hii ilibaini ukiukwaji wa haki ya kupata msaada wa kisheria na kuamuru malipo ya laki tatu (TZS 300,000) yamewekwa pamoja.

| JAMHURI YA BENIN | 1. Sébastien Germain Ajavon | | |
|---|---|---|---|
|  | **Shauri la Maombi Na. 013/2017** | **Shauri la Maombi Na. 062/2019** | **Shauri la Maombi Na. 065/2019** |
| | **Hukumu** ya tarehe 29 Machi 2019 kuhusu stahili na ya tarehe 28 Novemba 2019 kuhusu fidia. | **Hukumu** ya tarehe 4 Disemba 2020 kuhusu stahili na fidia. | **Hukumu** ya tarehe 29 Machi 2021 kuhusu stahili na fidia. |
| | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>**Vyombo vya habari vinaripoti kwamba** Nchi Mjibu Maombi imefanya mabadiliko kwenye sheria iliyoanzisha Mahakama ya CRIET na kuanzisha Mahakama ya Rufaa kama ilivyoagizwa kwenye hukumu. | Ibara za 3, 5, 7(1) (a), (b), (c), 14 na 26 za Mkataba wa Afrika na ibara za 14(3) (d), 14(5) na (7) za ICCPR. | Ibara za 2, 4, 5, 7(1), 10, 13(1), 26 za Mkataba wa Afrika; Ibara za 8 (1) (d) na 8(2) za ICESCR; 10(2), 17(1) za ACDEG; ibara ya 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora. | Ibara ya 30 ya Itifaki ya Mahakama ya Afrika na ibara ya 1 ya Mkataba wa Afrika. |
| | **Hatua kwa ajili ya fidia:** | **Hatua kwa ajili ya fidia:** | **Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| | Kuchukua hatua zote muhimu ili kufuta Hukumu Na. 007/3C. COR iliyotolewa na CRIET mnamo tarehe 18 Oktoba 2018 ili kufuta madhara yote na kuitaarifu Mahakama hii ndani ya miezi sita (6) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii.<br><br>Kumlipa Mleta Maombi faranga 36,330,444,947 za Afrika Magharibi kama fidia ya athari kubwa na jumla ya faranga 3,045,000,000 za Afrika Magharibi kama fidia ya madhara kimaadili ambayo yaliwapata mkewe, watoto wake watatu na yeye mwenyewe. | Kufuta ibara ya 27 (2) ya Sheria Na. 2018; Ibara za 1 na 2 za Sheria Mama Na. 2018; Sheria Na. 2019 – 39 na kufanya uchunguzi wote muhimu unaoweza kuwawezesha waathirika kupata haki zao za kulipwa fidia; kufuta vifungu vyote vinavyozuia haki ya kufanya mgomo, kuhakikisha kuna uhuru kwenye Mahakama ya Katiba na mfumo wa kimahakama. | Kutekeleza maagizo yaliyomo katika Hukumu inayohusiana na Shauri la Maombi Na. 013/2017. |
| | 2. XYZ | | |


<table>
<tr><td rowspan="6">Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:<br><br>Nchi Mjibu Maombi haikuwasilisha ripoti. Ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ya Mashauri ya Maombi Na. 059/2019 na 010/2020 uliisha tarehe 27 Februari 2021.</td><td>Shauri la Maombi Na. 059/2019</td><td>Shauri la Maombi Na. 010/2020</td></tr>
<tr><td>Hukumu ya 27 Novemba 2020 kuhusu stahili na fidia.</td><td>Hukumu ya 27 Novemba 2020 kuhusu stahili na fidia.</td></tr>
<tr><td>Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td><td>Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td>Ibara ya 13(1) ya Mkataba wa Afrika, ibara ya 17(1) ya ACDEG na ibara ya 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora.</td><td>Ibara za 9(1), 22(1), 23(1), na 26 za Mkataba wa Afrika; ya 10(2) ya ACDEG.</td></tr>
<tr><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td>Kuchukua hatua za kuoanisha muundo wa COS-LEPI ulingane na masharti ya Ibara ya 17 (2) ya ACDEG na ibara ya 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora kabla ya uchaguzi wowote.</td><td>Kuhakikisha Mahakama ya Katiba inakuwa huru; pia kufuta Sheria Na. 2019-40 iliyotungwa tarehe 1 Novemba 2019 inayohusu Katiba ya Jamhuri ya Benin na sheria zote zinazoendana nayo, hasa Sheria Na. 2019-43 inayohusu Kanuni za Uchaguzi na kumlipa Mleta Maombi faranga moja (1) ya Afrika Magharibi kama mfano wa malipo kufanyika.</td></tr>
<tr><td rowspan="10">Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:<br><br>Nchi Mjibu Maombi haikuwasilisha ripoti. Muda wa kufanya hivyo uliisha tarehe 27 Februari 2021.</td><td colspan="2">3. Éric Houngue</td></tr>
<tr><td colspan="2">Shauri la Maombi Na. 003/2020</td></tr>
<tr><td colspan="2">Hukumu ya tarehe 27 Novemba 2020 kuhusu stahili na fidia.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ibara ya 13(3) ya Mkataba wa Afrika, 10(2) ya ACDEG na ya UDHR.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Kufuta Sheria Na. 2019-40; kuzingatia kanuni ya maridhiano ya kitaifa yaliyoainishwa katika Ibara ya 10(2) ya ACDEG kwa ajili ya mabadiliko yoyote ya kikatiba; kuchukua hatua zote za kufuta Amri Na. 023/MJL/DC/SGM/DACPG/SA 023SGGG19 iliyotolewa kwa Wizara mtambuka mnamo tarehe 22 Julai 2019; kuchukua hatua zote za kukomesha na kuondoa athari zote za mabadiliko ya kikatiba.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td rowspan="13">Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:<br><br>Nchi Mjibu Maombi haikutoa ripoti yoyote. Ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti kwenye Shauri la Maombi Na. 024/2020 utakuwa tarehe .................. 2023.</td><td colspan="2">4. Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje</td></tr>
<tr><td colspan="2">Shauri la Maombi Na. 024/2020</td></tr>
<tr><td colspan="2">Hukumu kuhusu stahili na fidia ya tarehe 13 Juni 2023</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ibara za 5, 7(1)(b) za Mkataba wa Afrika na ya 15 ya Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Fidia:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Nchi Mjibu Maombi inaamriwa kuchukua hatua zote muhimu ili kufuta Amri Na. 023/MJL/DC/SGM/DACPG/SA 023SGGG19 iliyotolewa kwa Wizara mtambuka mnamo tarehe 22 Julai 2019 ndani ya miezi sita (6) kufuatia taarifa ya hukumu hii.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Kuhusu utekelezaji na utoaji wa ripoti</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| | Nchi Mjibu Maombi inaamriwa kuwasilisha Mahakamani, ndani ya miezi sita (6) kufuatia taarifa ya hukumu hii, ripoti juu ya hatua zilizochukuliwa kutekeleza kipengele (vii) cha Sehemu hii ya Uamuzi. |

| | |
|---|---|
| **JAMHURI YA IVORY COAST** | **1. Hatua za Ulinzi wa Haki za Binadamu** |
|  | **Shauri la Maombi Na. 001/2014** |
| | Hukumu ya tarehe **18 Novemba 2016** kuhusu stahili na ya tarehe **28 Septemba 2017** kuhusu tafsiri ya hukumu. |
| | |
| | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** |
| | Ibara 3(2), 13(1) na (2) za Mkataba wa Afrika; 10(3) na 17 za Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala; 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora; na 26 ya ICCPR. |
| | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi :**<br><br>Mnamo tarehe 28 Agosti 2019, Msajili alipokea barua pepe iliyotumwa kwa niaba ya Nchi Mjibu Maombi ambapo Nchi Mjibu Maombi ilielezea kuwa, kufuatia mashauriano na umma, ilikuwa imepitisha sheria mpya ya kurekebisha muundo wa Baraza la Usimamizi wa Uchaguzi. Kwa mujibu wa Nchi Mjibu Maombi, baada ya kufanya mabadiliko haya, inaona kwamba imetii hukumu ya Mahakama hii. Mnamo tarehe 19 Novemba 2019, Mleta Maombi aliwasilisha ripoti inayoeleza kuwa ingawa sheria hiyo ilirekebishwa ili kujumuisha taasisi zisizo za kiserikali, haikushughulikia ipasavyo suala la uhuru wa Tume ya Uchaguzi. Pia walihisi kuwa mchakato wa kufanya mabadiliko ya sheria haukuwa shirikishi.<br><br>Katika kujibu, Nchi Mjibu Maombi ilisisitiza kuwa ilishatekeleza kikamilifu hukumu ya Mahakama hii, kwamba ilikuwa imetunga sheria mpya ambayo inatoa uhuru kwa Tume ya Uchaguzi. Aidha, ilisema kuwa ilishauriana na wadau wote walio tayari kushiriki katika mchakato wa kurekebisha sheria. Mwisho, ilisema kuwa barua kutoka APDH haikuonesha kwa usahihi maoni ya | **Hatua kwa ajili ya fidia:**<br><br>Kufanya mabadiliko ya Sheria Na. 2014-335 ya 18 Juni 2014 inayohusiana na Tume Huru ya Uchaguzi ili iendane na mikataba iliyotajwa hapo juu ambayo kwayo ni mwanachama. |

<table>
<tr><td>Mleta Maombi kwani muundo wa ofisi yao umebadilika na mwandishi wa ripoti iliyowasilishwa Mahakamani hakuwa na haki ya kuzungumza kwa niaba ya APDH.</td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="9">Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:<br><br>Mnamo tarehe 1 Septemba 2020, Nchi Mjibu Maombi iliwasilisha ripoti yake ya muda juu ya utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa na Serikali. Mnamo tarehe 14 Septemba 2020, Waleta Maombi walisema katika ripoti yao kwamba walikuwa wanapinga tafsiri ya Nchi Mjibu Maombi kuhusu hukumu ya Mahakama hii. Nchi Mjibu Maombi iliombwa kujibu hoja za Waleta Maombi ndani ya siku tano (5). Mnamo tarehe 2 Novemba 2020, Msajili alipokea Ripoti ya Utekelezaji wa Nchi Mjibu Maombi na hoja za Waleta Maombi juu ya utekelezaji wa hukumu ya Mahakama hii. Katika ripoti yake ya utekelezaji, Nchi Mjibu Maombi inasema kuwa imetii amri ya Mahakama hii ya kufanya upya chaguzi kwenye Ofisi ya Tume ya Uchaguzi katika ngazi ya mtaa. Chaguzi hizi zilifanyika mwezi Agosti 2020. Kuhusu amri ya Mahakama hii juu ya mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa Tume za Uchaguzi na asasi za kiraia na vyama vya siasa, hasa vyama vya upinzani, Nchi Mjibu Maombi inawasilisha kwamba vyombo hivi tayari vinaamua kati yao nani wa kuteua, hata hivyo, wameombwa kuwasilisha vigezo vyao kwa Serikali ili Nchi Mjibu Maombi iweze kuwarasimisha. Nchi Mjibu Maombi imedokeza kuwa itawasilisha ripoti ya utekelezaji wa ziada mara tu mchakato huu wa urasimishaji utakapokamilika. Katika uchunguzi wao juu ya utekelezaji wa hukumu ya Mahakama hii, Waleta Maombi wanadai kuwa Nchi Mjibu Maombi haijatekeleza hukumu hii hata kidogo. Wanasimamia kwamba, kwa mujibu wa uamuzi wa Mahakama</td><td>2. Suy Bi Gohore</td></tr>
<tr><td>Shauri la Maombi Na. 044/2019</td></tr>
<tr><td>Hukumu ya tarehe 15 Julai 2020 kuhusu stahili na fidia.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td>Ibara za 3(7), 3(8), 13, 17 za Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala; na ya 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td>Kuchukua hatua muhimu kabla ya uchaguzi wowote ili kuhakikisha kuwa chaguzi mpya kwenye Ofisi zilizoundwa kwa kufuata muundo mpya wa chombo cha uchaguzi zinafanyika katika ngazi za mitaa; kuchukua hatua muhimu kabla ya uchaguzi wowote ili kuhakikisha kwamba mchakato wa kuteua wajumbe wa chombo cha uchaguzi kupitia vyama vya siasa, hasa vyama vya upinzani, pamoja na AZAKI, unaongozwa na vyombo hivi, kwa misingi ya vigezo vilivyowekwa, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kujiandaa, kushauriana, kufanya uchaguzi ikiwa ni lazima na kuwasilisha wagombea wenye sifa; na kutoa taarifa kwa Mahakama hii juu ya hatua zilizochukuliwa ndani ya miezi mitatu (3) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii.</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| hii, Tume ya Uchaguzi inapaswa kuundwa upya kwa kuzingatia wanachama wake walioteuliwa na vyama vya upinzani na asasi za kiraia. Muundo huu mpya hakukufanyika, kwa kuwa Nchi Mjibu Maombi ilialika chama kimoja tu cha upinzani kuteua mtu wa kukalia kiti cha Tume ya Uchaguzi. Hata hivyo, mbinu hii ya kuvialika vyama maalum vya kisiasa ilikiuka barua na amri ya Mahakama hii kwa kuwa maelekezo ya Mahakama hii yalikuwa ni kuhakikisha asasi za kiraia na vyama vya upinzani vinaamua miongoni mwao nani wa kumteua kuwa kwenye Tume ya Uchaguzi. Waleta maombi hao wanadai kuwa vyama vya upinzani viliitisha mikutano mbalimbali na kuteua wajumbe wapya wanne kuwa kwenye Tume Kuu ya Uchaguzi, lakini Nchi Mjibu Maombi haikukubali uteuzi huo. Kwa hiyo, Waleta Maombi wanashikilia kuwa, kwa kuwa Tume za Uchaguzi kwa ngazi za taifa na za mitaa hazikuundwa upya kwa mujibu wa hukumu ya Mahakama hii, uchaguzi uliofuata wa Ofisi ya Tume za Uchaguzi katika ngazi ya mitaa pia haukuzingatia hukumu ya Mahakama hii, hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba Tume za Uchaguzi za Mitaa zinaongozwa kwa asilimia 100 na wajumbe wa chama tawala. Mwisho, Waleta Maombi wanashikilia kuwa kwa kuwa Nchi Mjibu Maombi haikutekeleza amri ya Mahakama hii kabla ya uchaguzi wa 31 Oktoba 2020, uchaguzi huo unapaswa kuonekana ulikuwa si wa haki na batili. | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti yake ulikuwa tarehe 2 Mei 2022. Ripoti hiyo bado haijawasilishwa. | **3. Kouadio Kobena**<br>**Shauri la Maombi Na. 034/2017**<br>Hukumu ya tarehe 2 Disemba 2021 kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7(1) (d) ya Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| | Kumlipa Mleta Maombi jumla ya faranga milioni arobaini na tano (45,000,000) za Afrika Magharibi. |

| | |
|---|---|
| Ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti hiyo ni tarehe 22 Machi 2023 | **4. Kouassi Kouame Patrice na Baba Sylla**<br>**Shauri la Maombi Na. 015/2021**<br>Hukumu ya tarehe 22 Septemba 2022 kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa :**<br>Ibara za 6 na 13 za Mkataba wa Afrika, na ya 6 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuwalipa Waleta Maombi kiasi cha faranga milioni tatu, laki nne na themanini na tano elfu (3,485,000) za Afrika Magharibi. |
| | |
| **JAMHURI YA KENYA** | **Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu** |
|  | **Shauri la Maombi Na. 006/2012**<br>Hukumu ya tarehe **26 Mei 2017** kuhusu stahili na ya tarehe **23 Juni 2022** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 1, 2, 8, 14, 17(2) na (3), 21 na 22 za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi haikutoa ripoti juu ya hatua zilizochukuliwa kutekeleza hukumu. Ukomo wa muda wa kuwasilisha taarifa ulikuwa tarehe 26 Novemba 2017.<br><br>Hata hivyo, ikumbukwe kuwa taarifa zinazohusiana na uanzishwaji wa kikosi kazi kinachohusika na utekelezaji wa hukumu ya Mahakama hii kupitia Ilani katika Gazeti rasmi Na. GN/10944/2017 la tarehe 23 Oktoba 2017, kama ilivyotaarifiwa upya na Ilani Na. GN/2446/2018 ya tarehe 28 Februari 2018, ziko katika mfumo wa umma.<br><br>Mnamo tarehe 25 Januari 2022, Nchi Mjibu Maombi iliwasilisha ripoti juu ya utekelezaji wa hatua zilizoamriwa katika hukumu kuhusu stahili.<br><br>Ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti juu ya hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza Hukumu kuhusu fidia ni tarehe 23 Juni 2023. | Kumlipa Mleta Maombi shilingi milioni mia moja na hamsini na saba, laki nane na hamsini elfu (157,850,000) za Kenya zitakazowekwa kwenye mfuko wa maendeleo ya jamii; kuanzisha na kuhakikisha shughuli za Kamati ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo zinaanza kwa kishindo.<br><br>Kuchukua hatua zote muhimu za kisheria, kiutawala au nyingine ili kutambua, kwa kushauriana na Waogiek na / au wawakilishi wao, na kuonesha, kuainisha na kutoa hati miliki ya pamoja kwa ardhi ya mababu wa Ogiek ili kuhakikisha kuna matumizi na furaha kupitia uhakika wa kisheria.<br><br>Kuwa na mazungumzo na mashauriano kati ya Waogiek na / au wawakilishi wao, na vyama vingine husika kwa lengo la kukubaliana juu ya kama au kuruhusu wanufaika wa makubaliano kuendelea na shughuli zao kwa njia ya kukodisha na / au kugawana mrabaha na faida, na Waogiek, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Jamii. Pale ambapo maelewano hayawezi kufikiwa, Nchi Mjibu Maombi lazima iwafidie wahusika wengine na kurudisha ardhi kwa Waogiek.<br><br>Kuwatambuliwa kikamilifu Waogiek kama jamii ya wazawa wa Kenya na hili lifanyike ndani ya mwaka mmoja.<br><br>Kutambua, kuheshimu na kulinda haki ya Waogiek kuwa na mashauriano mema, kulingana na mila / desturi zao, juu ya miradi yoyote ya maendeleo, uhifadhi au uwekezaji kwenye ardhi ya mababu wa Waogiek.<br><br>Kuchapisha muhtasari rasmi wa Hukumu hii kwa Kiingereza. |

| | |
|---|---|
| | Kuhusu stahili, Nchi Mjibu Maombi inasema kuwa imechukua hatua za kisheria ili kutekeleza Sheria Na. 34 ya mwaka 2016 ya Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu na Sheria Na. 27 ya mwaka 2016 ya Ardhi ya Jamii inayoelekeza kuwa haki za ardhi za jamii lazima zisajiliwe kwa mujibu wa masharti yake na masharti ya Sheria ya Usajili wa Ardhi ya mwaka 2012. Aidha, Nchi Mjibu Maombi inaeleza kuwa hadi kufikia tarehe 25 Januari 2022, hatimiliki kumi (10) za ardhi za jamii zimeshapatikana: nne (4) katika Kaunti ya Pokot Magharibi, mbili (2) katika Kaunti ya Laikipia, moja (1) katika Kaunti ya Samburu na mbili (2) katika Kaunti ya Kajiado. Hadi kufikia tarehe 30 Oktoba 2020, jamii mbili: Llingwesi na Musul za Kaunti ya Laikipia wamefanikiwa kusajili ardhi yao ya jamii ikiwa na eneo la hekta 8675.5 na 2646.0.<br><br>- Kuhusu haki ya kutobaguliwa, Katika ripoti yao ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2019, Kabila la Waogiek liliainishwa kama kabila dogo chini ya kabila la Wakalenjin. Ripoti ya sensa ilitoa idadi ya Waogiek 52,596. Nchi Mjibu Maombi inatanabaisha kwamba imetambua kabila la Waogiek kama kabila lenye haki yake nchini Kenya.<br><br>- Kuhusu haki ya umiliki, Nchi Mjibu Maombi imeanzisha kikosi kazi cha kushughulikia utekelezaji wa uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Kikosi kazi kimewezesha mashauriano baina ya wadau wengi na jamii iliyoathirika na kuwasilisha mapendekezo na matokeo yake kwa mamlaka ya uteuzi mnamo Oktoba 2019. Mapendekezo ya kikosi kazi kwa sasa yanapitia hakiki za ndani (kuanzia Januari 25, 2022).<br><br>- Kuhusu haki ya utamaduni, ili kutekeleza kanuni za kikatiba za utamaduni za mwaka 2018, serikali, kwa kushirikiana na wanazuoni, asasi za kiraia na wadau wengine, iliandaa rasimu ya sera ya taifa ya utamaduni, ambayo inashughulikia maeneo mbalimbali makubwa yanayohusiana na utamaduni, kama vile maendeleo ya taifa, urithi wa taifa, lugha, taasisi za kitamaduni, familia, haki za binadamu, elimu, vyombo vya habari; elimu na utalii. |

| SERIKALI YA LIBYA | Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu |
|---|---|
|  | **Shauri la Maombi Na. 002/2013**<br>Hukumu ya tarehe **3 Juni 2016** kuhusu stahili<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 6 na 7 za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi haijawasilisha ripoti hadi sasa, ukomo wa muda wa kufanya hivyo ulikuwa tarehe 22 Novemba 2016. Hata hivyo, ripoti za vyombo vya habari ambazo hazijathibitishwa zinaonesha kwamba Bw. Kadhafi aliachiliwa huru mwaka 2017. | Kulinda haki zote za Bw. Kadhafi chini ya ibara za 6 na 7 za Mkataba wa Afrika kwa kukomesha mashauri ya jinai yaliyo kinyume na taratibu mbele ya Mahakama za ndani. |
| | |
| JAMHURI YA MALI | 1. Chama cha Maendeleo na Ulinzi wa Haki za Wanawake wa Mali na Taasisi ya Haki za Binadamu na Maendeleo Barani Afrika |
|  | **Shauri la Maombi Na. 046/2016**<br>Hukumu ya tarehe **18 Novemba 2018** kuhusu stahili.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 2, 2 (2), 6 (a) na (b), 21 (1) na (2) za Itifaki ya Maputo, 1 (3), 2, 3, 4 na 21 za Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto; 5 (a) na 16 (1) za Mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijaripoti juu ya hatua zilizochukuliwa wakati ukomo wa muda wa kufanya hivyo ulikuwa tarehe 11 Agosti 2020. | **Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuoanisha sheria iliyochafuliwa na mikataba ya kimataifa na kuchukua hatua muhimu kukomesha ukiukwaji wa sheria uliobainiwa. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa kutoa taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa kutekeleza hukumu juu ya fidia ulikuwa tarehe 24 | 1. Oumar Mariko<br>**Shauri la Maombi Na. 029/2018**<br>Hukumu ya tarehe **24 Machi 2022** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 7(1) (d) na 26 za Mkataba wa Afrika; 14(1) ya ICCPR; 17(1) ya Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala; na ya 3 ya Itifaki ya ECOWAS ya Demokrasia na Utawala Bora. |

| | |
|---|---|
| Septemba 2022. Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti juu ya hili. | |
| | **Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| | Kumpa Mleta Maombi jumla ya faranga milioni moja (1,000,000) za Afrika Magharibi; kurekebisha sheria zinazosimamia Mahakama ya Katiba kwa kuongeza vifungu vyenye kufuata kanuni ya kusikiliza pande zote, vifungu vinavyohusiana na utaratibu wa kuwafuta uanachama wajumbe wa Mahakama hiyo, ndani ya miaka mitatu (3) kuanzia kutangazwa kwa hukumu hii; kuchukua hatua zote muhimu kutekeleza kikamilifu wajibu wake wa kuhakikisha kuna uhuru wa Mahakama ya Katiba, ndani ya miaka miaka mitatu (3) kuanzia kutangazwa kwa hukumu hii; kuchukua hatua zote muhimu, kwa hali yoyote kabla ya uchaguzi wowote, kufuta ibara za 27 na 28 za Sheria ya Uchaguzi ndani ya miaka mitatu (3) kuanzia kutangazwa kwa hukumu hii; kuchukua hatua zote muhimu ili kutekeleza kikamilifu wajibu wake wa kuanzisha na kuimarisha vyombo huru na visivyo na upendeleo vya uchaguzi, ndani ya miaka mitatu (3) kuanzia kutangazwa kwa hukumu hii. |
| | |
| **JAMHURI YA MALAWI** | **Harold Mbalanda Munthali** |
|  | **Shauri la Maombi Na. 022/2017** |
| | Hukumu ya tarehe **23 Juni 2022** kuhusu stahili na fidia. |
| | |
| | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** |
| | Ibara za 1, 3(2), 7(1) na 7(1) (a) za Mkataba wa Afrika. |
| | |
| | **Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti yake bado haujaisha, na ukomo utakuwa tarehe 23 Disemba 2022. | Kumlipa Mleta Maombi kwacha za Malawi milioni mia mbili na tisa (209,000,000). |
| | |
| **JAMHURI YA RWANDA** | **1. Ingabire Victoire Umuhoza** |
|  | **Shauri la Maombi Na. 003/2014** |
| | Hukumu ya tarehe **24 Novemba 2017** kuhusu stahili na ya tarehe **7 Disemba 2018** kuhusu fidia. |
| | |
| | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:** |
| | Ibara za 7(1) (c), 9(2) za Mkataba wa Afrika na ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) |
| | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi haikuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa hukumu licha | **Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| | Kumlipa Mleta Maombi jumla ya faranga milioni kumi, laki mbili na themanini na tano elfu (10,285,000) za Rwanda. |
| | **2. Kennedy Gihana na wenzake** |
| | **Shauri la Maombi Na. 017/2015** |
| | Hukumu ya tarehe **28 Novemba 2019** kuhusu stahili na fidia. |

<table>
<tr><td rowspan="12">ya kumalizika kwa muda wa mwisho wa kufanya hivyo tarehe 16 Septemba 2018 kwa Shauri la Maombi Na. 003/2014, tarehe 1 Agosti 2020 kwa Shauri la Maombi Na. 017/2015 na tarehe 27 Aprili 2021 kwa Shauri la Maombi Na. 012/2017.<br><br>Nchi Mjibu Maombi iliijulisha Mahakama hii kuwa inasitisha ushirikiano wote na Mahakama hii.</td><td></td></tr>
<tr><td>Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td>Ibara za 12(2) na 13(1) za Mkataba wa Afrika.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td>Kumlipa kila Mleta Maombi kiasi cha faranga laki nne na sitini na tano elfu (465,000) za Rwanda.</td></tr>
<tr><td>3. Léon Mugesera</td></tr>
<tr><td>Shauri la Maombi Na. 012/2017</td></tr>
<tr><td>Hukumu ya tarehe 27 Novemba 2020 kuhusu stahili na fidia.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td>Kumlipa Mleta Maombi jumla ya faranga milioni thelathini na tano (35,000,000) za Rwanda; kuteua daktari wa kujitegemea kutathmini hali ya afya ya Mleta Maombi na kuamua hatua zinazohitajika kumsaidia.</td></tr>
<tr><td>JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA</td><td>1. Chama cha Wanasheria Tanganyika na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Mchungaji Christopher R. Mtikila</td></tr>
<tr><td rowspan="7"></td><td>Mashauri ya Maombi Na. 009 na 011 ya 2011 (Kesi ya pamoja)</td></tr>
<tr><td>Hukumu ya tarehe 14 Juni 2013 kuhusu stahili na ya 13 Juni 2014 kuhusu fidia.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:</td></tr>
<tr><td>Ibara za 2, 3, 10 na 13(1) za Mkataba wa Afrika.</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td>Hatua kwa ajili ya fidia:</td></tr>
<tr><td>Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:<br><br>Nchi Mjibu Maombi iliwasilisha ripoti tatu kuhusiana na suala hili mnamo tarehe 17 Aprili 2015, 18 Januari 2016 na 3 Januari 2017. Nchi Mjibu Maombi imesema kuwa utekelezaji wa hukumu ya Mahakama hii ulitokana na matokeo ya kura ya maoni juu ya rasimu ya Katiba na kwamba Katiba ilitoa wagombea huru katika uchaguzi wa serikali za mitaa, ubunge na urais. Mnamo tarehe 3 Januari 2017 Nchi Mjibu Maombi iliiarifu Mahakama hii kuwa kura ya maoni bado ilikuwa inasubiriwa.<br><br>Mnamo tarehe 16 Oktoba 2020, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Chama cha Wanasheria Tanganyika walifungua shauri Mahakamani wakiomba amri inayotaka Nchi Mjibu</td><td>Kuchukua hatua zote za kikatiba, kisheria na nyingine zinazofaa ndani ya kipindi cha muda mwafaka ili kukomesha ukiukwaji wa sheria uliobaniwa na kuchapisha muhtasari wa hukumu.</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| Maombi kuchukua hatua za kutekeleza hukumu itekelezwe. Shauri hili limesajiliwa bila majibu hadi sasa. | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi :**<br><br>Kuhusu stahili - Nchi Mjibu Maombi ilieleza kuwa amri ya kuchukua hatua zote muhimu ndani ya muda muafaka ili kurekebisha makosa ya jinai, ukiondoa kuanza tena kwa utetezi na kufunguliwa tena kwa kesi hiyo, haikutekelezwa na kwa hivyo Nchi Mjibu Maombi iliwasilisha ombi kwa lengo la kutafsiri hukumu. Hukumu hiyo ilitolewa na Mahakama hiyo Septemba 28, 2017. Kwa hali yoyote, Nchi Mjibu Maombi haijawasilisha ripoti ya kufuatilia ili kuonesha hatua ambazo imechukua kujibu hukumu hii kuhusu tafsiri.<br><br>Kuhusu fidia – Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti juu ya utekelezaji wa hukumu juu ya fidia licha ya kumalizika kwa ukomo wa muda hukusu hili ambao ulikuwa tarehe 5 Januari 2020. | **2. Alex Thomas**<br>**Shauri la Maombi Na. 005/2013**<br>Hukumu ya tarehe **20 Novemba 2015** kuhusu stahili na ya tarehe **4 Julai 2019** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7(1) (a), (c) na (d) ya Mkataba wa Afrika na 4(3) (d) ya ICCPR.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi shilingi za kitanzania milioni tatu na laki tano (3,500,000) na shilingi za Kitanzania milioni moja (1,000,000) kwa wanafamilia wake waliotambuliwa kama waathirika wasio wa moja kwa moja. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Kuhusu stahili – Nchi Mjibu Maombi imewasilisha ripoti zake juu ya utekelezaji wa hukumu kuhusu stahili ambazo inasema kuwa wadau wamefahamishwa juu ya masharti ya sheria inayohusiana na msaada wa kisheria na wajibu wao wa kuwajulisha watuhumiwa/washitakiwa juu ya uwezekano wa kupata msaada huo. Sheria ya Msaada wa Kisheria ilichapishwa katika Gazeti rasmi la Serikali mwezi Machi 2017. Nchi Mjibu Maombi ilifafanua kuwa wakati Mahakama hii inaamuru kutoa msaada wa kisheria kwa waombaji katika kesi zinazosubiri dhidi yao mbele ya Mahakama za ndani, Mahakama Kuu ilikuwa tayari imetoa uamuzi juu ya rufaa zao za jinai, ikiwa ni pamoja na Rufaa Na. 47 na 48 za 2014. Katika hukumu | **3. Wilfred Onyango Nganyi**<br>**Shauri la Maombi Na. 006/2013**<br>Hukumu ya tarehe **18 Machi 2016** kuhusu stahili na ya tarehe **4 Julai 2019** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa :**<br>Ibara ya 7(1) (a), (c) na (d) ya Mkataba wa Afrika na 14(3) (d) ya ICCPR.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Katika hukumu kuhusu stahili, Mahakama hii iliamuru Nchi Mjibu Maombi kuchukua hatua zote muhimu, ndani ya muda unaofaa, kuharakisha na kukamilisha kesi zote za rufaa za jinai kuhusu Waleta Maombi mbele ya Mahakama za ndani. Kuhusu fidia, iwalipe Waleta Maombi na wanafamilia wao kiasi cha dola za Kimarekani sitini na tano elfu na mia tano (65,500) na shilingi za Kitanzania milioni tatu (3,000,000), mtawalia. |

| | |
|---|---|
| yake iliyotolewa mnamo tarehe 10 Disemba 2015, Mahakama Kuu ilitupilia mbali rufaa ya Waleta Maombi. Nchi Mjibu Maombi imeeleza katika ukurasa wa 11 wa Hukumu ya Mahakama hiyo kwamba baadhi ya Waleta maombi walipewa Wakili, ambaye ni Bw. Mwesijo, ingawa baadaye alijitoa mwenyewe kwenye kesi. Nchi Mjibu Maombi ilieleza zaidi kwamba Waleta Maombi waliwasilisha mbele ya Mahakama ya Rufani taarifa yao ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Nchi Mjibu Maombi inasubiri kupokea taarifa ya rufaa za Waleta Maombi. Nchi Mjibu Maombi haijawasilisha ripoti juu ya hukumu kuhusu fidia. Kuhusu fidia: Nchi Mjibu Maombi imeshindwa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa hukumu kuhusu fidia licha ya muda wa kufanya hivyo kufikia ukomo tarehe 5 Januari 2020. | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi :**<br><br>Kuhusu stahili – Nchi Mjibu Maombi ilionesha kuwa wadau wa mfumo wa haki za jinai walifahamishwa juu ya masharti ya Sheria ya Msaada wa Kisheria na wajibu wao wa kuwajulisha watuhumiwa / washitakiwa juu ya uwezekano wa kupata msaada huo. Nchi Mjibu Maombi pia ilieleza kwamba Sheria ya Msaada wa Kisheria ya 2017 ilishapitishwa. Sheria hii inasimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji, inatambua watu wenye uelewa wa kawaida wa sheria, inafuta Sheria ya Msaada wa Kisheria upande wa Utaratibu wa Jinai na kusaidia juu upande wa masuala yahusianayo. Nchi Mjibu Maombi pia iliomba ufafanuzi juu ya fidia kutokana na ukiukwaji huo wa sheria, ambao ulitolewa na Mahakama hii mnamo tarehe 28 Septemba 2017. Nchi Mjibu Maombi haijawasilisha ripoti ya ufuatiliaji juu ya suala hili.<br><br>Kuhusu fidia – Nchi Mjibu Maombi haikuwasilisha ripoti juu ya utekelezaji | **4. Mohamed Abubakari**<br>**Shauri la Maombi Na. 007/2013**<br>Hukumu ya tarehe **6 Juni 2016** kuhusu stahili na ya **4 Julai 2019** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7 ya Mkataba wa Afrika na 14 ya ICCPR.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi jumla ya shilingi za Kitanzania milioni nne na laki tano (4,500,000). |

| | |
|---|---|
| wa Hukumu licha ya muda wa kufanya hivyo kufikia ukomo tarehe 5 Julai 2020. | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi :**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti licha ya muda wa kuwasilisha ripoti kufikia ukomo tarehe 21 Septemba 2020.<br>Mnamo tarehe 24 Februari 2020, Mleta Maombi aliwasilisha barua Mahakamani akiomba iingilie kati utekelezaji wa hukumu ya Septemba 21, 2018. Mahakama hii iliituma barua hiyo kwa Nchi Mjibu Maombi na kuiomba iwasilishe maoni yake juu ya suala hilo. Ukomo wa muda wa kuwasilisha maelezo ya Nchi Mjibu Maombi ulikuwa tarehe 23 Mei 2020 bila Nchi Mjibu Maombi kufanya hivyo. | **5. Diocles William**<br>**Shauri la Maombi Na. 016/2016**<br>Hukumu ya tarehe **21 Septemba 2018** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7(1) na (1) (c) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Nchi Mjibu Maombi inaamuriwa kupitia upya shauri, kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Mkataba wa Afrika na viwango vingine vyovyote vya kimataifa vya haki za binadamu, ndani ya miezi sita (06), na kuhitimisha kesi hiyo ndani ya kipindi cha muda unaofaa, ambao kwa hali yoyote hautazidi miaka miwili kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi :**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa muda wa kufanya hivyo ulikuwa tarehe 14 Juni 2019. | **6. Armand Guehi**<br>**Shauri la Maombi Na. 001/2015**<br>Hukumu ya tarehe **7 Disemba 2018** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 1, 5 na 7(1) (d) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa kwa Mleta Maombi jumla ya dola za Marekani elfu mbili na mia tano (2,500). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa muda wa kufanya hivyo uliisha tarehe 2 Oktoba 2019. Mleta Maombi amewasilisha maombi mara nyingi Mahakamani kwa lengo la kuhakikisha Nchi Mjibu Maombi inafuata hukumu ya Mahakama hii. Maombi yote hayo ya Mleta Maombi yameshawasilishwa kwa Nchi Mjibu Maombi ili ijibu hoja ndani ya siku thelathini (30). Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kujibu hoja umeisha bila chochote kufanyika.<br><br>Mnamo tarehe 5 Machi 2021, Mleta Maombi aliiandikia Mahakama hii barua | **7. Lucien Ikili Rashidi**<br>**Shauri la Maombi Na. 009/2015**<br>Hukumu ya tarehe **28 Machi 2019** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 4, 5, 7(1) (d) na 12(1) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi jumla ya shilingi za Kitanzania milioni kumi na moja (11,000,000); kuchukua hatua zote muhimu ili kuhakikisha kwamba kuna ufuatiliaji wa kina kama ilivyo katika shauri hili unafanywa kwa umakini kwa kuzingatia vema wajibu wake kimataifa. |

| | |
|---|---|
| iliyoeleza kuwa alikuwa ameomba mwakilishi wa Burundi katika Umoja wa Afrika na Rais wa Burundi kuingilia kati na kuwezesha utekelezaji wa hukumu hiyo. | |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti yake ulikuwa tarehe 30 Agosti 2020.<br><br>Mnamo tarehe 29 Septemba, 2020, Wakili wa Waleta Maombi aliwasilisha ombi Mahakamani la kutaka msaada wa kifedha ili kuwawezesha kufuatilia vema utekelezaji wa hukumu. Msajili alikiri kupokea barua ya Waleta Maombi na kumjulisha Wakili kwamba sera ya sasa ya Mahakama hii kuhusu msaada wa kisheria haitoi msaada kwa wakili kufuatilia utekelezaji wa hukumu zake. | **8. Ally Rajabu na wenzake**<br>**Shauri la Maombi Na. 007/2015**<br>Hukumu ya tarehe **28 Machi 2019** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 4, 5, 7(1) (d) na 12(1) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa kila Mleta Maombi shilingi za Kitanzania milioni nne (4,000,000) kama fidia ya madhara ya kimaadili; kuondoa ulazima wa adhabu ya kifo katika Kanuni yake ya Adhabu; kupitia upya shauri kuhusu hukumu na kuchapisha hukumu ndani ya miezi mitatu (3). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti yake ulikuwa tarehe 30 Agosti 2020.<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijatoa ripoti.<br><br>Mleta Maombi alituma barua Mahakamani akiiomba isimamie utekelezaji wa hukumu ambayo ilikuwa imetoa. | **9. Robert John Penessis**<br>**Shauri la Maombi Na. 013 ya 2015**<br>Hukumu ya tarehe **28 Machi 2019** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara 1, 5, 6, 12 za Mkataba wa Afrika; na 15 za UDHR.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta mapombi shilingi za Kitanzania milioni kumi na tano (15,000,000) kama fidia ya madhara ya kimaadili kwake na mama yake na shilingi za Kitanzania laki tatu (300,000) kwa kila mwezi wa kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii hadi alipoachiwa huru. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado halijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti hii ulikuwa tarehe 8 Februari 2021. | **10. Nguza Viking na Johson Nguza**<br>**Shauri la Maombi Na. 006/2015**<br>Hukumu ya tarehe **23 Machi 2018** kuhusu stahili na ya tarehe **8 Mei 2020** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br><br>Ibara ya 1 na 7(1) (c) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumpatia Mleta Maombi wa kwanza shilingi za Kitanzania milioni ishirini (20,000,000) na kwa Mleta Maombi wa pili shilingi za Kitanzania milioni tano (5,000,000); kuchapisha hukumu ndani ya miezi mitatu (3) kuanzia |

| | |
|---|---|
| | tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii, kwenye tovuti rasmi za Mahakama za ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, kama kipimo cha kuonesha kuridhika, na kuhakikisha machapisho haya yanapatikana kwa angalau mwaka mmoja (1). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi mjibu maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 31 Januari 2021. | **11. Ambrose Cheusi**<br>**Shauri la Maombi Na. 004/2015**<br>Hukumu ya tarehe **26 Juni 2020** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara 7(1) (c) na 7(1) (d) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi jumla ya shilingi za Kitanzania milioni tano laki saba na ishirini na tano elfu (5,725,000) ; kuchapisha hukumu ndani ya miezi mitatu (3) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii, kwenye tovuti rasmi za Mahakama za ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, kama kipimo cha kuonesha kuridhika, na kuhakikisha machapisho haya yanapatikana kwa angalau mwaka mmoja (1). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado halijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti hii ulikuwa tarehe 31 Januari 2021. | **12. Jebra Kambole**<br>**Shauri la Maombi Na. 018/2018**<br>Hukumu ya tarehe **15 Julai 2020** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 2, 3(2) na 7(1) (a) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuchukua hatua zote muhimu za kikatiba na kibunge, ndani ya kipindi cha muda unaofaa, kwa namna yoyote ile usiozidi miaka miwili (2), kufanya mabadiliko kwenye ibara ya 41(7) ya Katiba yake ili iendane na masharti ya Mkataba wa Afrika, ili kukomesha ukiukwaji wa ibara ya 2 na 7(1) (a) ya Mkataba huu; kuchapisha hukumu ndani ya miezi mitatu (3) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii, kwenye tovuti rasmi za Mahakama za ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, kama kipimo cha kuonesha kuridhika, na na kuhakikisha machapisho haya yanapatikana kwa angalau mwaka mmoja (1). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 30 Machi 2021. | **13. Kennedy Owino na mwenzake**<br>**Shauri la Maombi Na. 003/2015**<br>Hukumu ya tarehe **28 Septemba 2018** kuhusu stahili na ya **30 Septemba 2021** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 1, 6, 7(1), 7(1) (c) na 22 za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa kila Mleta Maombi shilingi za Kitanzania milioni tano (5,000,000) kama fidia ya madhara ya kimaadili waliyopata; kuwaachia huru Waleta Maombi. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:** | **14. Amini Juma**<br>**Shauri la Maombi Na. 024/2016**<br>Hukumu ya tarehe **30 Septemba 2021** kuhusu stahili na fidia. |

| | |
|---|---|
| Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 30 Machi 2021. | **Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara 1, 4, 5 na 7(1) (d) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuwalipa Waleta Maombi shilingi za Kitanzania milioni nne (4,000,000); kuondoa ulazima wa adhabu ya kifo kwenye Kanuni yake ya Adhabu; kupitia upya shauri linalohusu hukumu na kuchapisha hukumu ndani ya miezi sita (6). |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 2 Juni 2021. | **15. Anudo Ochieng Anudo**<br>**Shauri la Maombi Na. 012/2015**<br>Hukumu ya tarehe **22 Machi 2018** kuhusu stahili na ya tarehe **2 Disemba 2021** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7 ya Mkataba wa Afrika; 14 ya ICCPR, na 15(2) ya UDHR.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuwalipa Waleta Maombi jumla ya shilingi za Kitanzania milioni sabini (70,000,000); kuchukua hatua zote muhimu za kurejesha haki za Mleta Maombi kwa kumruhusu arejee katika nchi yake, kumhakikishia ulinzi wake na kuripoti Mahakamani ndani ya siku arobaini na tano (45) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii; kufanya mabadiliko ya sheria yake ili kuwapa raia wake nafuu ya kisheria pale kunapokuwa na changamoto kuhusu uraia wao; kuchapisha hukumu. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 22 Juni 2022. | **16. Thobias Mango na mwenzake**<br>**Shauri la Maombi Na. 005/2015**<br>Hukumu ya tarehe **11 Mei 2018** kuhusu stahili na ya tarehe **2 Disemba 2021** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara za 1, 6, 7 (1),7 (1) (c) na 22 za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kuwalipa Waleta Maombi shilingi za Kitanzania milioni mbili na laki tano (2,500,000) kwa kila mwathirika wa moja kwa moja na shilingi za Kitanzania milioni nne na laki tano (4,500,000) kwa kila mwathirika asiye wa moja kwa moja. |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Nchi Mjibu Maombi bado haijawasilisha ripoti, ingawa ukomo wa muda wa kuwasilisha ripoti ulikuwa tarehe 2 Juni 2022. | **17. Robert Richard**<br>**Shauri la Maombi Na. 035/2016**<br>Hukumu ya tarehe **2 Disemba 2021** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7(1) (d) ya Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi shilingi za Kitanzania milioni tano (5,000,000). |
| | **18. Mgosi Mwita Makungu**<br>**Shauri la Maombi Na. 006/2016** |

| | |
|---|---|
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti utakuwa tarehe 23 Disemba 2022. | Hukumu ya tarehe **17 Disemba 2018** kuhusu stahili na ya **23 Juni 2022** kuhusu fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 7(1) (a) ya Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:** |
| **Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**<br><br>Ukomo wa muda wa Nchi Mjibu Maombi kuwasilisha ripoti utakuwa tarehe 23 Machi 2023. | **19. Joseph John**<br>**Shauri la Maombi Na. 005/2018**<br>Hukumu ya tarehe **22 Septemba 2022** kuhusu stahili na fidia.<br><br>**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**<br>Ibara ya 6 na 7(1) (c) za Mkataba wa Afrika.<br><br>**Hatua kwa ajili ya fidia:**<br>Kumlipa Mleta Maombi shilingi za Kitanzania laki sit (600,000). |

## MASHAURI AMBAYO MAHAKAMA ILIBAINI UKIUKWAJI WA HAKI YA UTETEZI NA KUAMURU HATUA SAWA ZICHUKULIWE

| Na. ya Ombi | Jina la Mleta Maombi | Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa | Tarehe ya hukumu kuhusu stahili na fidia | Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi |
|---|---|---|---|---|
| 020/2016 | 1. Anaclet Paulo | Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba wa Afrika ikisomwa kwa pamoja na ibara ya 14(3) ya ICCPR | 21 Septemba 2018 | Nchi Mjibu Maombi haijawasilisha ripoti |
| | 2. Minani Evarist | | 21 Septemba 2018 | |
| 025/2016 | 3. Kenedy Ivan | | 28 mars 2019 | |
| 025/2015 | 4. Majid Goa | | 26 Septemba 2019 | |
| 028/2015 | 5. Kalebi Elisamehe | | 26 Juni 2020 | |
| 011/2015 | 6. Christopher Jonas | | Hukumu ya tarehe 28 Septemba kuhusu stahili na ya tarehe 25 Septemba 2020 kuhusu fidia | |
| 033/2015 | 7. James Wanjara | | 25 Septemba 2020 | |
| 022/2016 | 8. Mussa Zanzibar | | 26 Februari 2021 | |
| 054/2016 | 9. Mhina Zuberi | | 26 Februari 2021 | |
| 010/2015 | 10. Amir Ramadhani | | Hukumu ya tarehe 11 Mei 2018 kuhusu stahili na ya tarehe 25 Juni 2021 kuhusu fidia | |
| 032/2015 | 11. Kijiji Isiaga | | Hukumu ya tarehe 28 Septemba 2017 kuhusu stahili na ya tarehe 25 Juni 2021 kuhusu fidia | |
| 008/2016 | 12. Masoud Rajabu | | 25 Juni 2021 | |
| 001/2016 | 13. Chrizostom Benyoma | | 30 2021 | |
| 047/2016 | 14. Ladislaus Onesmo | | 30 Septemba 2021 | |
| 026/2015 | 15. Hamis Shaban Hamis Ustadh | | 2 Disemba 2021 | |
| 005/2016 | 16. Sadick Marwa Kisase | | 2 Disemba 2021 | |
| 013/2016 | 17. Stephen John Rutakikirwa | | 24 Machi 2022 | |
| 032/2016 | 18. Hoja Mwendesha | | 13 Juni 2023 | |
| 058/2016 | 19. Niyonzima Augustine | | 13 Juni 2023 | |

| JAMHURI YA TUNISIA | Ibrahim Ben Mohammed Ben Belghuith |
|---|---|



**Shauri la Maombi Na. 017/2021**

Hukumu ya tarehe **22 Septemba 2022** kuhusu stahili na fidia.

**Ukiukwaji wa sheria uliobainiwa:**

Ibara za 1, 7(1) (a) za Mkataba wa Afrika zikisomwa kwa pamoja na ibara za 26 na 13 za Mkataba huu.

**Hatua kwa ajili ya fidia:**

Kufuta Matamko ya Rais Na. 2021-117 ya tarehe 22 Septemba 2021 na Na. 69, 80, 109 ya tarehe 26, 29 Julai na 24 Agosti 2021 na Na. 137 na 138 ya tarehe 11 Oktoba 2021 na kurejesha demokrasia ya kikatiba ndani ya miaka miwili (2) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii; kuchukua hatua zote muhimu kuhakikisha Mahakama ya Katiba inafanya kazi na kuondoa vikwazo vyote vya kisheria na kisiasa vinavyozuia lengo hili, ndani ya miaka miwili (2) kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa hukumu hii.

**Hatua zilizochukuliwa na Nchi Mjibu Maombi:**

Mnamo tarehe 2 Machi 2023, Nchi Mjibu Maombi iliwasilisha ripoti inayoonesha kuwa uamuzi wake wa Mahakama ulikuwa wa kinadharia. Hii ni baada ya Katiba ya 2022 kuanza kufanya kazi na kufanyika kwa uchaguzi wa wabunge mnamo tarehe 17 Disemba 2022 na 29 Januari 2023 na kwamba, mara tu Baraza la Wawakilishi litakapochukua madaraka, Tamko la Rais Na. 117 litakuwa limepitwa na wakati. Kuhusu suala la Mahakama ya Katiba, Nchi Mtoa Majibu ilidokeza kuwa Rais wa Jamhuri alikuwa amemuagiza Waziri Mkuu kuandaa rasimu ya sheria kwa ajili ya Mahakama ya Katiba ambayo itahakikisha Mahakama ina nguvu na kwa mantiki hiyo, wamechukua hatua muhimu za kuanzisha Mahakama ya Katiba na wataijulisha Mahakama hii mara tu sheria itakapotangazwa.

Katika kujibu, Mleta Maombi anashikilia kwamba hukumu haijatekelezwa kwa sababu Tunisia haijarejesha demokrasia ya kikatiba. Ameongeza kwamba uongozi wa sasa unaamini haujapoteza demokrasia na hivyo unaelekea kutotekeleza uamuzi wa Mahakama hii. Hivyo, anaiomba Mahakama hii kuchukua hatua za kuhakikisha utekelezaji wa hukumu yake unafanyika.

# MKUTANO WA SITA WA MAHAKAMA ZA AFRIKA

*****************************************************************

# KUKUZA HAKI ZA BINADAMU BARANI AFRIKA:

# CHANGAMOTO NA FURSA ZA KUJUMUISHA KATIKA MAHAKAMA ZA NDANI SHERIA ZA KANDA NA KIMATAIFA ZINAZOHUSIANA NA HAKI ZA BINADAMU

**************************************************

## JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA WATU WA ALGERIA

***************************************

## ALGIERS

***************************

## 20-22 NOVEMBA 2023

****************

**TAARIFA YA MWISHO**

1. Chini ya usimamizi wa Umoja wa Afrika (UA), Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Mahakama) iliandaa Mkutano wa Sita wa Mahakama (Mkutano wa Mahakama) chini ya kaulimbiu: "Changamoto na fursa za kujumuisha katika mahakama za ndani sheria za kanda na kimataifa zinazohusiana na haki za binadamu." kuanzia tarehe 20-22 Novemba 2023 mjini Algiers, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria..

2. Mkutano wa Mahakama ulifunguliwa rasmi na Mhe. Nadir Larbaoui, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, aliyemwakilisha Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria. Katika hotuba yake, Waziri Mkuu alisisitiza juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri katika kukuza na kulinda haki za binadamu. Waziri Mkuu alisisitiza msimamo wa Umoja wa Afrika kuhusu suala la Palestina na kulaani uhalifu dhidi ya binadamu unaofanywa huko Gaza, na kuelezea mshikamano usio na masharti wa Afrika kwa watu wa Palestina.

3. Wazungumzaji wengine katika sherehe ya ufunguzi walikuwa ni pamoja na Mhe. Abderrachid Tabi, Waziri wa Sheria wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Mhe. Jaji Imani D. Aboud, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, na Mhe. Balozi Mohamed Salem Khalil Kaimu Mwanasheria wa Umoja wa Afrika.

4. Mkutano wa Mahakama ulihudhuriwa na Majaji Wakuu, Marais wa Mahakama/Mabaraza ya Kikatiba au wawakilishi wao kutoka Nchi thelathini na saba (37) Wanachama wa Umoja wa Afrika pamoja na wadau na wabia ambao ni pamoja na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (Tume ya Banjul), Kamati ya Afrika ya Wataalamu wa Haki na Ustawi wa Mtoto (Kamati ya Wataalamu), Mahakama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAT), Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR), Mahakama ya Umoja wa Nchi za Kiarabu za Afrika ya Kaskazini, Mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) (Mahakama ya ECOWAS), Mahakama ya Umoja wa Kiuchumi na Fedha wa Afrika Magharibi, na Umoja wa Mamlaka za Kikatiba barani Afrika, na Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Ujerumani GmbH) (GIZ).

5. Mkutano wa Sita wa Mahakama uliwaleta pamoja washiriki mia moja thelathini na saba (137) kutoka taasisi mbalimbali za mahakama za kitaifa na kimataifa pamoja na vyombo vya Umoja wa Afrika. Pia ulihudhuriwa na wadau wengine kama vile vyombo vya habari, asasi za kiraia, mashirika ya kitaaluma/taasisi na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali.

6. Lengo kuu la Mkutano wa Sita wa Mahakama za Umoja wa Afrika lilikuwa ni kutoa fursa kwa majaji wa mahakama za kitaifa na kanda na wadau wengine kujadili changamoto na fursa zinazohusiana na kuoanisha sheria za kanda na kimataifa za haki za binadamu katika mahakama za ndani za Afrika. Pia ulilenga kuchunguza, kujadili, na kuchambua mwelekeo wa Protokali ya Maputo, elimu endelevu ya sheria ya haki za binadamu kuhusu haki za wanawake ndani ya mfumo wa haki za binadamu wa Afrika, na umuhimu wa kujenga uelewa

miongoni mwa Majaji Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, kuhusu umuhimu wa kuoanishwa kwa sheria hii katika mifumo yao ya kisheria ya ndani.

7. Mkutano wa Mahakama pia uliwapa washiriki fursa ya kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu sheria zinazoibuka kutoka kwenye sheria zinazohusiana na uhalali wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

8. Mkutano Mahakama ulisisitiza umuhimu wa Mkutano wa Mahakama na haja ya ushirikiano endelevu kati ya mahakama za kimataifa, kanda na kitaifa ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu katika bara hili.

9. Vikao tisa vya Mkutano wa Mahakama vilijikita kwenye:

   i. Taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mkutano uliopita wa Mahakama;
   ii. Jukumu na umuhimu wa sheria za haki za binadamu za kanda na kimataifa;
   iii. Changamoto zinazozikabili mahakama za ndani katika kujumuisha sheria za haki za binadamu;
   iv. Utendaji bora katika utumiaji wa viwango vya kanda na kimataifa vya haki za binadamu;
   v. Kuimarisha ushirikiano kati ya mahakama za kanda na za ndani;
   vi. Kujenga uwezo na maendeleo ya kitaaluma kwa majaji na wanasheria;
   vii. Miaka 20 ya Protokali ya Maputo;
   viii. Kuridhia na kutumika ndani ya nchi kwa hati za haki za binadamu za kanda na kimataifa barani Afrika;na
   ix. Kubadilishana uzoefu kuhusu sheria zinazoibuka kutoka kwenye sheria zinazohusiana na haki za kiuchumi, kiutamaduni na kijamii na haki ya maendeleo, tafakari kuhusu changamoto za kisasa na matarajio ya baadaye

10. Baada ya siku tatu za majadiliano ya wazi, wajumbe wa Mkutano wa Mahakama walitoka na maazimio yafuatayo:

11. **Kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Mkutano uliopita wa Mahakama, wajumbe** waliihimiza Mahakama ya Afrika na Kituo cha Haki za Binadamu (CHR), Chuo Kikuu cha Pretoria kushirikiana na kuratibu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo na wadau husika, ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa (AIIL), Taasisi ya Mahakama ya Afrika (JIFA) , Chuo Kikuu cha CapeTown, vituo vya haki za binadamu katika nchi mbalimbali, mtandao wa Afrika wa wakufunzi wa mahakama na vituo vya mafunzo ya mahakama za kitaifa, Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, miongoni mwa wengine, kuanzisha kozi za mafunzo zilizoandaliwa maalumu kwa maafisa wa mahakama wa Afrika na wanasheria kwa kutumia lugha zote za kazi za Umoja wa Afrika.

12. Mkutano wa Mahakama pia *ulitoa wito* kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa ushirikiano na Mahakama ya Afrika, na kwa kuzingatia Azimio la Baraza la Utendaji EX.CL/Dec.1153 (XL) la Februari 2022, kuanzisha Mtandao wa Afrika wa Mahakama bila kuchelewa.

13. **Kuhusu jukumu na umuhimu wa sheria za kanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu -** Mkutano wa Mahakama *ulizihimiza* mahakama za kanda na kimataifa kutekeleza jukumu lao la kutunga sheria za kimataifa na kuzifanya

zipatikane kwa kuanzisha kanzidata ya utafutaji ya kielektroniki kuhusiana na maamuzi yao yote katika lugha zote za kazi za Umoja wa Afrika;

14. *Pia uliitaka* Mahakama ya Afrika na mahakama mbalimbali za kitaifa na kanda za Afrika ziendelee kuimarisha ubadilishanaji wa maarifa, uzoefu na utendaji bora kupitia mikutano ya mahakama inayofanyika mara kwa mara na taratibu nyinginezo.

15. **Kuhusu changamoto zinazozikabili mahakama za ndani katika kujumuisha sheria za haki za Binadamu –** Mkutano wa Mahakama ulizihimiza mahakama za kitaifa kujifunza kutoka kwa wenzao na kutafuta njia bunifu, inapobidi, za kutumia moja kwa moja sheria na kanuni za kimataifa za haki za binadamu;

16. **Kuhusu utendaji bora katika kutumia viwango vya haki za binadamu vya kanda na kimataifa**: Mkutano wa Mahakama *ulizihimiza* Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kuimarisha utawala wa sheria kwa kuhakikisha na kulinda uhuru wa mahakama.

17. Pia, Mkutano wa Mahakama *ulitoa wito kwa* maafisa wa mahakama katika ngazi ya kitaifa kutumia kanuni za kimataifa za haki za binadamu katika mahakama za ndani, na mahakama za kitaifa *zilihimizwa* kutumia viwango vya sheria za kimataifa na kanuni *zinazojulikana* katika kuamua kesi zilizo mbele yao.

18. **Kuhusu kuimarisha ushirikiano kati ya mahakama za kanda na za ndani**: Mkutano wa Mahakama ulipendekeza kufanyika kwa maboresho ya Protokali inayoanzisha Mahakama ya Afrika ili kuruhusu mahakama kuu za nchi mbalimbali za Afrika kuomba ushauri kutoka kwenye Mahakama ya Afrika.

19. **Kuhusu kujenga uwezo na maendeleo ya kitaaluma kwa majaji na wanasheria:** Mkutano wa Mahama ulizitaka Nchi Wanachama kuweka kipaumbele katika mafunzo ya majaji kuhusu haki za binadamu kupitia uanzishwaji wa vyuo vya mafunzo ya ngazi ya juu, pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya mafunzo endelevu kwa majaji;

20. Mkutano wa Mahakama ulipendekeza kuanzishwa kwa mitandao, kulingana na misingi ya lugha na mila za kisheria, kwa madhumuni ya kushirikishana kwa urahisi sheria za haki za binadamu.

21. **Kuhusu miaka 20 baada ya Protokali ya Maputo,** Mkutano wa Mahakama ulitoa wito kwa Mataifa kumi na moja (11) ya Afrika yaliyosalia kuridhia Protokali ya Maputo na ulizihimiza Nchi Wanachama kutumia ndani ya nchi na kutekeleza kikamilifu Protokali ya Maputo.

22. Mkutano pia ulibainisha wahamasishaji ili kusaidia kuridhiwa kwa Protokali ya Maputo katika nchi ambazo bado hazijaridhia hati hiyo.

23. Mkutano ulizihimiza Nchi kutekeleza maamuzi yote ya mahakama za kimataifa, pamoja na mahakama za ndani, zinazoshughulikia haki za wanawake.

24. Pia *ulizitaka* mahakama za kimataifa na kanda kunukuu mara kwa mara Protokali ya Maputo, Maoni ya Jumla kuhusu vifungu vyake na hati nyingine za kisheria, katika maamuzi yao yanayohusiana na haki za wanawake.

25. **Kuhusu Kubadilishana uzoefu kuhusiana na sheria zinazoibuka kutoka kwenye sheria zinazohusiana na haki za kiuchumi, kiutamaduni na kijamii na haki ya maendeleo, tafakari kuhusu changamoto za kisasa na matarajio ya baadaye**. Mkutano wa Mahakama *ulizihimiza kwa dhati* mahakama za kimataifa ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Afrika kushirikiana kwa karibu na mahakama za kitaifa kwa kuzipa taarifa kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;

26. *Ulitoa wito* kwa Mahakama ya Afrika na mahakama za kitaifa na kanda kuendeleza ubadilishanaji wa maarifa, uzoefu na utendaji bora kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

27. Washiriki waliazimia kuwa Mkutano wa Saba wa Mahakama za Afrika utafanyika mwaka 2025 katika mahali na tarehe itakayoamuliwa.

28. Washiriki walitoa shukrani zao kwa Mhe. Abdelmajid Teboun, Rais wa Algeria na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria kwa ukarimu wao na huduma walizopatiwa ili kuhakikisha Mkutano wa Sita wa Mahakama za Afrika unafanikiwa.

29. Washiriki pia waliishukuru Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu kwa kuandaa Mkutano wa Sita wa Mahakama pamoja na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, Umoja wa Ulaya na GIZ kwa msaada wao.

**RASIMU YA UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA MWAKA 2023 YA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Baraza la Utendaji,**

1. **LINATAMBUA**Ripoti ya Shughuli za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) kwa kipindi cha tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba 2023;

2. **INAPOKEA** maandalizi yenye mafanikio ya Majadiliano ya 6 ya Mahakama ya Umoja wa Afrika huko Algiers, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria kutoka kuanzia tarehe 20 hadi 22 Novemba 2023, na Inatambua Taarifa ya Mwisho iliyopitishwa mwishoni mwa Majadiliano hayo.

3. **Inatoa wito** kwa Mahakama ishirikiane na Tume ya Umoja wa Afrika na vyombo na taasisi nyingine husika za Umoja wa Afrika, pamoja na taasisi husika za kitaifa na kikanda ili kuhakikisha utekelezaji wa Taarifa ya Mwisho.

4. Inapokea uamuzi wa …. kuteua Watu Maalumu… kulingana na Uamuzi wa Baraza la Utendaji…., na inazialika Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kuchukua hatua za kuteua Watu Maalumu

5. **INAZINGATIA KWA MASIKITIKO** kwamba zaidi ya miongo miwili baada ya kupitishwa kwake, ni nchi thelathini na nne tu (34) Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zimeridhia Itifaki na nane tu (8) kati ya Nchi Wanachama 34, zimeweka Azimio linalohitajika chini ya Kifungu cha 34 (6), ikiruhusu watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasilisha kesi moja kwa moja kwenye Mahakama ya Afrika;

6. **INAZIPONGEZA** Nchi thelathini na nne (34) Wanachama wa Itifaki, ambazo ni; Algeria, Benin, Burkina Faso, Burundi, Kameruni, Chad, Côte d'Ivoire, Komoro, Congo, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Kenya, Libya, Lesotho, Madagascar, Mali, Malawi, Msumbiji, Mauritania, Mauritius, Nigeria, Niger, Rwanda, Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi, Senegal, Tanzania, Togo, Tunisia na Uganda.

7. **PIA INAWAPONGEZA** Nchi Wanachama nane (8) ambazo zimeweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, nchi hizo ni: Burkina Faso, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Malawi, Mali, Niger na Tunisia.

8. **INAZIALIKA** Nchi Wanachama ambazo hazijafanya hivyo, zikubali Itifaki, na kuweka Azimio linalohitajika chini ya Kifungu cha 34 (6) cha Itifaki.

9. **IBAINISHA** kwa masikitiko kiwango cha chini cha uzingatiaji wa maamuzi ya Mahakama na **INATOA** wito wa uzingatiaji kamili wa maamuzi ya Mahakama, na **INAZIALIKA** Nchi Wanachama ambazo hazijafanya hivyo, ziteue watu maalumu wa kitaifa ili kuhakikisha ufuatiliaji mzuri kuhusu masuala yote yanayohusiana na Mahakama, ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa maamuzi ya Mahakama.

10. **Inatoa wito** kwa Tume, kwa kushirikiana na Mahakama ya Afrika na vyombo vingine husika vya Umoja wa Afrika na Taasisi, kufanya utafiti kuhusu ya hali ya kuzingatia maamuzi ya vyombo vya haki za binadamu vilivyoanzishwa na Umoja wa Afrika, na kutoa mapendekezo thabiti, ikiwa ni pamoja na, ikiwa ni lazima, uteuzi wa msimamizi wa Umoja wa Afrika wa haki za binadamu na watu.

11. **INAMSIHI** Mwenyekiti wa Tume, kulingana na Maamuzi ya awali ya Baraza la Utendaji, yaani, (EX.CL/Des.973 (XXXI); (EX.CL/Des.994 (XXXII); EX.CL/Des.1044 (XXXIV); (EX.CL/Des.1064 (XXXV); na (EX.CL/Des.1079), achukue hatua zote muhimu za kutekeleza Mfuko wa Msaada wa Kisheria kwa Vyombo vya Haki za Binadamu vya AU, na kulingana na hayo, **ANAWAALIKA** na **KUZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa Umoja, pamoja na wadau wengine wa haki za binadamu katika bara, kutoa michango ya hiari ya ukarimu kwa ajili ya Mfuko ili kuhakikisha uendelevu na mafanikio yake.

12. **Inapokea** uamuzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuanza ujenzi wa majengo ya kudumu ya Mahakama.

13. **INAIOMBA** Mahakama, kwa kushirikiana na RPC na AUC, kuripoti katika Kikao kijacho cha Kawaida cha Baraza la Utendaji mnamo Juni/Julai 2024, juu ya utekelezaji wa Uamuzi huu.

**AFRICAN UNION UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs | Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-02-15

# Activity report of the African Court on Human And Peoples' Rights (AfCHPR)

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10532

*Downloaded from African Union Common Repository*